Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 172 | JUMADULAWWAL 1434AH | MACHI 2013 | AMMAN 1392 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Sema: Enyi watu wa Kitabu, hamko juu ya cho chote mpaka msimamishe Taurati na Injili, na yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu. Na bila shaka yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidisha wengi wao katika uasi na kufuru. Basi usihuzunike juu ya watu wanaokufuru. (5:69).

Sheikh Kaluta Amri Abedi na Jiji la Cairo

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam

Jiji la Cairo ni lenye historia ya kusisimua. Inasimuliwa kuwa hapo ndipo chimbuko la ustaarabu ambao umeenea duniani kote. Fani ya kuandika, utengenezaji wa kalenda, utaalamu wa kilimo cha umwagiliaji inasemekana yote haya yalizaliwa katika jiji hili. Ni katika jiji hili ndipo Nabii Mussa (as) alipopanga mikakati ya kuwaokoa Waisraeli kutoka utumwani. Gamal Abdul Nasser naye katika jiji hili akishirikiana na akina Zakaria Muhyuddin walipanga mipango ya kutokomeza ubwenyenye. Na tarehe 23 Juni 1955 Taifa la kimapinduzi la Misri likazaliwa. Akiwa Cairo, Nasser akaandika kitabu maarufu "Philosophy of the Revolution"



Sheikh Kaluta Amri Abedi

Katika kitabu hicho akaeleza kuwa Misri ni sehemu ya Afrika na kuwa haitapa usingizi asilani hadi bara la Afrika limekuwa huru na kurudishiwa heshima yake. Na akafafanua kuwa Misri itaongozwa na maduara matatu yaani kujali sana Afrika, kujali uhusiano wao na Uarabuni na kujali uhusiano wao na Asia. Tamko hili likafuatwa kwa vitendo vya kimapinduzi, Cairo ikawa ni kimbilio la wapigania uhuru. Abdulkarimu wa Moroco, Ferhat Abbasi wa Algeria, Saleh Ben Yousuf wa Algeria wote hao wakapata hifadhi mjini Cairo. Vyama vya siasa vya Uganda, Somalia, Afrika ya Kusini, Kenya, Mozambique, Niger, Nigeria, Chad, Zanzibar zikafungua ofisi zao katika jiji hilo.

Gazeti la Al-Akhram chini ya Mohamedi Heikal yule muandishi maarufu wa vitabu vya *Autumn of Fury, The Cairo Documents, The Road to Ramadhani, Sphinx and Commissar* and *The return of the Ayyatollah* likawa sauti kwa wale ambao hawana sauti. Radio huru ya Afrika ikaanzishwa ambayo ikafanya kazi ya kueneza habari njema za uhuru na heshima ya Mwafrika. Al-Ahzar chuo kikuu kilichoanzishwa karne 13

Endelea uk. 2

Kiongozi wa Waislam Duniani ampongeza Papa Francis I

Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya imetoa pongezi kwa Kanisa Katoliki na wafuasi wake kote duniani kufuatia uchaguzi wa Papa mpya, Mtakatifu Francis I.



Papa Francis I, Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, aliyechaguliwa hivi karibuni kuliongoza Kanisa hilo

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya na Khalifa Mtukufu wa Tano wa Masihi Aliyeahidiwa (as), Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a amesema:

"Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Papa Francis I na kwa Wakatoliki kote duniani. Mwenyezi Mungu ajaalie kuchaguliwa kwa Papa mpya kulete baraka sio tu kwa Wakristo bali kwa watu wote duniani kote. Mwenyezi Mungu ajaalie Papa huyu mpya aliongoze Kanisa katika mafundisho ya kweli ya Ukristo." Amin.

Zawadi kwa Malkia Victoria: Jazba ya Hadhrat Ahmad katika Mahubiri

Na Mwandishi wetu - Dar es salaam

Mapitio ya vitabu viwili - "Zawadi kwa Kaisari" na "Nyota ya Kaisari" vilivyoandikwa na Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) vimepitiwa na Mahmood Hamsin Mubiru.

Mwaka 1897 Malkia Victoria alisherehekea miaka 60 ya kuwa kwenye kiti cha kifalme nchini Uingereza. Ilikuwa ni sherehe ya kukata na shoka kutokana na ukweli kwamba Malkia huyo alikuwa amejenga jamii yenye kuheshimu haki za binadamu, uhuru wa kuabudu na kusukuma mbele chachu ya maendeleo. Uingereza ilikuwa ni nchi ambayo jua lake halikuweza kutua lenye kuongoza katika viwanda, hadi kupata lakabu ya "Karakana ya dunia". Uingereza ni nchi iliyotoa wavumbuzi katika uwanja wa sayansi na waandishi mahiri wa fasihi.

Kutokana na mafanikio hayo Masihi Aliyeahidiwa (as) alimtumia barua ya hongera Malkia Victoria kwa kuandika vitabu viwili ambavyo tumevitaja hapo juu. Kabla hatujatizama maudhui ya vitabu hivyo viwili tunadhani ni jambo la msingi kutizama angalau kwa akali maisha ya Malkia Victoria na mafanikio yake katika utawala wake wa miaka 60 ulioanza mwaka 1837 alipokuwa na umri wa miaka 18 hadi alipofariki mwaka 1901.

Victoria binti wa Duke wa Kent, mmoja wa watoto wa George III alimrithi mjomba wake Wiliam mwaka 1837 akiwa binti wa miaka 18. Malkia Victoria alipendwa sana na wananchi wake kwa mapenzi yake kwa watu na ukarimu uliochanganyika na huruma. Wakati anatawazwa kuwa Malkia Lord Rolle aliyekuwa na miaka 80 alianguka kwenye ngazi alipokuwa anakwenda kumpongeza Malkia Victoria. Malkia Victoria aliamka kutoka kwenye kiti chake na kumsaidia mzee huyo Lord Rolle kusimama. Tendo hili linaeleza vizuri khulka ya Malkia Victoria. Mapenzi hayo yalizidi kwani alipata bahati ya kuolewa na bwana mwenye hekima na busara. Prince Consort Wasare Cobung huyu alikuwa ni Mjerumani aliyeonyesha tabia ya Kijerumani ya kupenda kazi na kuheshimu kazi.

Mwaka 1861 Prince Consort alifariki na kumuacha Malkia Victoria katika lindi la majonzi.

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Jihadhari Nao

Mataifa ya Magharibi kwa kiwango kikubwa na cha kushtua wamekubuhu, wamebobea na wameshamiri katika kutengeneza na kuuremba uongo wao. Wamezama katika uongo kiasi hiki ya kwamba wameanza kuamini uongo walioutengeneza kwa mikono yao. Ni maradhi ya aina yake kuuamini uongo ulioutunga wewe mwenyewe.

Tutatoa mifano miwili ili kuthibitisha madai yetu haya. Wakieleza sababu zilizowaleta Afrika, watu wa Magharibi wanadai ya kwamba jambo hilo lilitokana na huruma yao, na utu wao uliowasukuma kuliokoa bara la giza lililokuwa limezama katika ushenzi na ukosefu wa maendeleo. Kwao Afrika haikuwa na utamaduni, haikuwa na sheria, hakukuwa na kanuni. Ulikuwa ni mkusanyiko wa watu waliopungukiwa katika kila maana ya neno hilo. Hapana shaka huo ulikuwa uongo dhahiri. Ulitungwa makusudi ili kuhalalisha maovu waliyoitendea Afrika.

Ni kweli Waswahili hawakukosea waliposema, 'Ukitaka kumuua nyani usimtizame usoni'. Hivyo walijenga hoja ya kudhihirisha kwamba sisi hatukuwa watu na hivyo yote waliyotutendea ilikuwa ni ihsani kubwa kwetu. Huo ulikuwa uongo uliofurutuada.

Jicho la historia linatueleza kwamba sababu zilizowaleta katika Afrika sio kwamba walitupenda sana sisi bali walijipenda wao zaidi. Ubepari katika hatua hii ambao ni chimbuko la nchi za Magharibi ulifika katika hatua ulipohitaji kupanuka na kwenda nje ya mipaka ya nchi za Magharibi. Na safari zote hizo, hazikuwa kwenda kwenye safari ya fungate, bali kilichowasukuma zaidi ni mahitaji ya malighafi yaliyohitajika katika viwanda vyao, soko ambapo wangeweza kuuza vitu vyao, mahali pa kuwekeza na hatimaye kuwapa hifadhi akina yakhe wa Ulaya ambao hawakuwa na mbele wala nyuma. Kwa ujumla maisha yote ya nchi za Ulaya yamejengwa kwenye msingi huo wa uongo.

Hata baadhi ya matatizo yanayosemekana kwamba yapo duniani kwa hakika yametengenezwa na wao wenyewe. Mathalani, dunia haina uhaba hata kidogo wa mafuta lakini wao wameficha mafuta mengi nchini kwao, wanakwenda katika nchi masikini duniani wanakomba mafuta yao na kuendeleza umasikini wao. Yote hiyo ni sehemu kubwa ya uongo ambao ni jiwe kuu la msingi la utamaduni wao.

Miaka kumi iliyopita Rais George Bush wa Marekani na Waziri Mkuu wa Uingereza Tony Blaire walijipakia katika mtumbwi wa uongo na wakaanza kuvinjari. Waliiambia dunia tena kwa viapo kuwa Rais Sadam Husseni alikuwa na silaha za maangamizi na hivyo alitakiwa achakazwe barabara. Hakuna chombo kilichobaki nyuma katika kueneza uongo huo, Luninga, Radio, Magazeti wimbo ulikuwa huo huo. Dunia yote kwa sauti moja ilipinga na kutaka ushahidi wa tuhuma hizo. Lakini wao wakaweka pamba masikioni mwao na wakaendelea na utamaduni wao wa uongo na kuhakikisha kwamba wametimiza uongo wao kwa vitendo.

Nani asiyefahamu maafa makubwa yaliyotokea Iraq? Nchi yenye miaka mingi ya maendeleo na utamaduni ikateketezwa vilivyo. Watu wengi wakauwawa, majengo yakaharibiwa, sehemu muhimu za kihistoria zikateketezwa na sababu kubwa ni kukumbatia utamaduni wa uongo.

Majeshi ya Marekani na Uingereza yaliingia Iraq kwa dhamira moja tu ya kutafuta silaha za maangamizi. Mpaka wa leo hata harufu ya silaha hizo haijasikika. Lakini sisi hatushangai, kwa sababu aliyezoea vya kunyonga, vya kuchinja haviwezi.

Ni huzuni kubwa wakati huu tunapotimiza miaka 10 ya ukatili na dhuluma kubwa iliyofanywa na mataifa haya mawili ambayo yamejengeka kwenye msingi wa uongo. Ni huzuni kubwa kwamba waliopika uongo huo bado wanaendelea kupeta na wala hawana fikra za kuomba radhi. Watamuomba nani radhi? Ni huzuni kubwa ya kwamba hatuwaoni katika Mahakama ya kimataifa (The Hague), wanachukuliwa wengine. Hii inatukumbusha shairi la Sheikh Kaluta Amri Abedi aliyesema;

Mambo ya kale na leo, pindi ukiyatizama
Kwa juu maogeleo, au kwa mbizi kuzama
Ni ajabu kwa mbineo, pande za mti kwachama
Ndovu akavwila wima, sisimizi akakwama

Sisi sisimizi wa dunia tumekwama na tunafahamu fika sababu zilizofanya mataifa hayo yaishambulie Iraq. Ni masuala ya kulipizana kisasi, kwani zilikuwepo fikra kwamba Sadam Hussein alikuwa na mikakati ya kumuua baba yake George Bush. Kwa vyovyote itakavyokuwa ni aibu kwamba dunia imeuacha uongo huu utekelezwe kwa vitendo.

Suala la kujiuliza ni kwamba, ni lini basi dunia itaunganika pamoja na kwa sauti moja ilaani wale wanaosema uongo na bila uoga wawaeleze kwamba waongo wana mwisho mbaya?

Sheikh Kaluta Amri Abedi na Jiji la Cairo

Kutoka uk. 1

zilizopita kikawa chemchem ya fikra za kuleta mwelekeo mpya katika Afrika.

Ni jiji hili la Cairo lenye uhusiano wa aina yake na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Ni katika jiji hili ndipo Sheikh Kaluta alipomkabidhi Gamal Abdul Nasser tafsiri ya Qur'an Tukufu katika Kiswahili, akamkabidhi pia tafsiri hiyo hiyo ya Kiswahili Mkuu wa chuo wa Al-Ahzar Mufti Mohamedi Shaltut ambae alitoa fat'wa kuwa Nabii Issa (as) amefariki na katika Cairo ndipo Sheikh Amri alipoandika mashairi yake maarufu 'Raha' na 'Siri ya mafanikio'. Na ni katika jiji hili alipouona mwili wa Firauni wa enzi za Mussa na ni hapo alipoanza ule ugonjwa ambao ulitimiza kwake ile aya ya Qur'an Tukufu '*Kila nafsi itaonja mauti*'.

Mwaka 1961 akiwa Mbunge wa Kigoma, Sheikh Kaluta Amri Abedi alipewa mualiko na serikali ya Misri kutembelea nchi hiyo. Sifa za Sheikh Kaluta Amri Abedi zilikuwa zimewafikia wabunge wengi wa Misri na wao walikuwa wana hamu ya kumsikia mwenyewe. Mkutano wa vyama vya siasa pamoja na serikali huru za kiafrika za wakati ule ulifanyika mjini Dar es salaam, mwisho mwa kikao chao ulifanyika mkutano wa hadhara katika viwanja vya Jangwani. Umati ulikuwa umefurika. Sheikh Amri alikuwa amepewa jukumu la kutafsiri hotuba ya Mjumbe wa Misri ambayo ilikuwa katika Kiarabu. Ujumbe wa Misri ulifurahi sana na uwezo wake mkubwa wa Kiarabu na hivyo walimkaribisha aitembelee Misri.

Tazama Bwana huyu alivyojitahidi kutanguliza dini. Alipotua jijini Cairo alipokeleewa kwa furaha na wenyeji wake. Warabu wanao utamaduni wa kuwa wakarimu kwa wageni. Licha ya ile ratiba waliokuwa wamempangia walimuuliza iwapo atakuwa na jambo la ziada alilokuwa anataka kufanya akiwa Cairo. Katika mizigo yake alikuwa amebeba tafsiri 3 za Qur'an Tukufu katika lugha ya Kiswahili. Hivyo aliomba kuonana na Gamal Abdul Nasser Rais wa Misri na Mkuu wa chuo cha Al-Ahzar Mufti Mohamedi Shautit.

Rais Gamal Abdul Nasser alipokea tafsiri hiyo ya Qur'an Tukufu katika Kiswahili kwa furaha kubwa, baadae alimpa Msahafu wa pili Sheikh Mohamedi Shautut Mkuu wa chuo cha Kiislam maarufu sana ulimwenguni cha Al-Ahzar. Sheikh Kaluta Amri Abedi mara baada ya kujitambulisha katika lugha ya Kiarabu akampa zawadi ya Qur'an Tukufu katika Lugha ya Kiswahili. Mufti alimuomba Sheikh Kaluta Amri Abedi awasomee kidogo Qur'an Tukufu. Maofisa alioongozana nao pamoja na Walimu akiwemo Mufti walishangaa sana kumuona Sheikh Kaluta Amri Abedi akisoma Qur'an Tukufu vizuri. Kila neno analitamka kwa ufasaha hasa. Hawakusita kumsifu na kumwambia kweli yao kuwa anawashinda baadhi ya Waarabu wengi katika usomaji wa Qur'an Tukufu.

Naye Sheikh Mohamedi Shautut akampa zawadi Sheikh Amri ya vitabu viwili. *Al-Fatawa* na *Taujahot* vitabu ambavyo vimeandikwa na mtaalamu huyo. Sheikh Amri alishuhudia mwenyewe maneno ya Mwenyezi Mungu katika Qur'an Tukufu. Katika jumba la makumbusho Sheikh Amri aliweza kuona kiwiliwili cha Firauni aliyekuwepo wakati wa Mussa. Kiwiliwili hicho kimehifadhiwa licha ya kuwa maelfu ya miaka mingi sana imepita tangu Firauni amekufa.

Mwaka 1962, mwaka mmoja baada ya uhuru wa Tanganyika, Sheikh Kaluta Amri Abedi aliteuliwa na mwanafunzi mwenzie waliokuwa wote pamoja shuleni Tabora - Mwalimu Julius K. Nyerere kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora. Sielewi hali ya Sheikh Kaluta ilikuwaje siku anaapishwa kuwa Mkuu wa Mkoa. Ambapo alidharauliwa na kutukanwa. Bila shaka fikra zake zilikwenda hadi kwenye tungo zake za mwaka 1953 "Miye mwerevu miye, mwisho mtajionea" na "Kuzamako huibuka"

Bishara zote alizokuwa anaambiwa na mwalimu wake -Sheikh Mubaraka Ahmad (HA) zilikuwa zimetimia mbele ya macho yake. Jiwe lililokataliwa na Waashi ndio sasa limekuwa jiwe kuu la pembeni. Mwenyezi Mungu Ana njia zake nyingi. Lakini Sheikh Kaluta hakulimbuka, alifahamu ya kwamba yeye alikuwa ni mtumishi na sio Bwana. Na katika hotuba yake ya kwanza akiwa Mkuu wa Mkoa alieleza wazi wazi; "Nimekuja hapa nikiwa mtumishi wenu, milango ya Ofisi yangu iko wazi kwenu ninyi nyote na wakati wote". Hayo ndiyo mafunzo ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kuhusu kiongozi. Kiongozi ni Mtumishi wa watu, kama kuna njaa yeye anakula mwisho. Na likiwepo la kufanywa yeye anakuwa mstari wa mbele. Sahaba mmoja wa Mtume (saw) wakati wanachima handaki alimuonesha njaa aliyokuwa nayo kwa mawe mawili aliyokuwa amefunga tumboni mwake. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alimuonesha mawe matatu aliyokuwa nae pia amefunga kwa ajili hiyo hiyo ya njaa.

Majivuno ilikuwa ni tabia mbali na Sheikh Amri. Alielewa vizuri historia. Alielewa mwisho mbaya waliopata viongozi waliokuwa wenye kibri na majivuno. Shairi alilopenda kulisoma mara kwa mara ni la rafiki yake Shaaban Robert "Maisha". Na alipenda kukariri ubeti ufuatao;

Walokuwa wakivuma, kama mvumo wa mlio
Dunia ikatetema, kwa kukunjwa kama tao
Mashujaa wana kama, katika mashambulio
Pia wamekwisha zama, pamoja na sifa zao

Mwaka huo alikuwa mgeni kwa mara ya pili wa Serikali ya Misri. Aliwekwa kwenye hoteli ya kifahari iliyokuwa inatizamana na mto Nile. Kila kitu anachokihitaji binadamu alikuwa nacho. Mara alisikia kengele akaitikia, na mtu akamletea gazeti la *Mapenzi ya Mungu* na habari nyingine za Jumuiyya. Haraka alikwenda kwenye bustani za Washairi na kukuta kuwa shairi la Sahib yake Maliki Abdallah Mbungiro (Watachoka) likiwa linamuhusu yeye Sheikh Amri. Maliki Abdallah Mbungiro alikuwa mshairi maarufu wa huko Rusende -Rufiji. Alikuwa na imani thabiti juu ya Jumuiyya Ahmadiyya na alionja ile raha ya kuteswa kwa sababu ya kupokea haki. Huku akitabasamu na bila kujali yaliyompata aliwahi kuiumba; 'Ibilisi kuwa dini sote tungesalimika'.

Nimzungupule huyu aliyekuwa anamkumbusha Sheikh Amri kwani kukumbushana ni amri ya Mwenyezi Mungu. Alimkumbusha hivi;

Sote tumo furahani, habarizo kutufika
Kwa kusoma gazetini, cheo cha kubadilika
Kwenda kuketi jimboni, twakuombea fanaka
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Sisi sote twaamini, nyoyo hazina mashaka
Kwani kwetu si mgeni, Umeya uliishika

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Sheikh Kaluta Amri Abedi na Jiji la Cairo

Kutoka uk. 2

Mambo mengi ya mjini, mara yakabadilika
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Yale mambo chinichini, yaliyopata kuzuka
Hayakuwa na thamani, waropo waliropoka
Ni ya kuvunja imani, ya watu walokushika
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Walivalia miwani, wakubwa kushughulika
Wakagundua kiini, nia ya wale vizuka
Wakabadili plani, husuda isije zuka
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Twakuombea Manani, Mola wetu Mtukuka
Maisha mema kitini, Tabora ulikofika
Pia na mambo ya dini, usije kughafilika
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Mtukuze Mola wako, Yeye mbele Kumuweka
Awe ndiyo nguzo yako, kila litalo kufika
Jema au la sumbuko, Mkimbilie haraka
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Watini wazaituni, mwenyewe wayakumbuka
Hata Nabi Sulemani, kitini enzi kashika
Aliishi kwa amani, nawe iwe kadhalika
Rabi Akupe hekima na huruma kadhalika

Siku ya kupokea gazeti hilo ilikuwa tarehe 17 July 1962 na siku hiyo hiyo kutokana na nasaha aliyopewa na sahibu yake aliingia ndani na akaanza kuandika shairi la kumpa maelezo rafiki yake Maliki Abdallah Mbungiro (Watachoka).

Shairi la Watachoka lilimgusa kiasi hiki ya kwamba alitafuta kalamu yake ilipokuwa na karatasi akaanza kudondosha mistari yenye utamu wa asali. Hili ni moja ya mashairi yake bora, na shairi ambalo limejikusanyia sifa zote za shairi bora. Hakuna neno lililolazimishwa ni mtiririko kutoka mwanzo hadi mwisho. Uteuzi wa maneno unaburudisha nafsi na maana hasa ya shaihri la kiswahili inapatikana katika utungo huu. Mafundisho ya dini ya Islam ni kwamba lazima tuanze na neno '*Bismillahi Rahmaanir Rahim*' hiyo ni aya ya Qur'an Tukufu, na ndivyo alivyoanza Sheikh Amri katika shaihri lake. Aya hii ina ujumbe mzito hapa zimeelezwa sifa mbili za Allah zinazoendesha dunia. Allah Anasifa ya Rahman. Chochote ambacho nafsi inahitaji kwa maendeleo ya kimwili na kiroho kimekwisha tayarishwa kwa kupitia sifa hii. Tumekuta tayari ardhi ipo ili tuweze kuishi, jua, mwezi kwa ajili ya mwanga. Hewa kwa ajili ya kupumua, maji kwa ajli ya kunywa, kitabu kwa ajili ya muongozo. Hakuna anayeweza kusema kuwa haya yote yamepatikana kutokana na baraka za juhudi zake au kwamba katika maisha ya kabla kuna aliyoyafanya kustahili yote aliyopewa. Na hakuna ubaguzi katika neema hii. Tajiri, maskini, mweupe, mweusi wote wanapata. Hivyo Sheikh Amri anaanza na dua kubwa mno. Anaanza kwa jina la Allah Ambaye ni Muumbaji wa kila kitu. Ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa. Amekariri sifa inayoonesha kwamba Mwenyezi Mungu ni Rahman kwa kutupatia kila kitu hata kabla hatujamuomba kwani ni mara nyingi hatujui hata tunachokihitaji. Hata namna ya kuomba tunafundishwa. Sifa ya pili ni Rahim ambayo mtu anavuna alichopanda. Mwanadamu anapata sawa na bidii aliyoweka "Manijitahada wajada" - Mwenye kujitahidi anapa.

Sheikh Amri anasema anaanza na Mwenyezi Mungu Mwenye sifa hizi mbili zinazoiendesha dunia. Sheikh Amri anaanza shairi kwa kuzingatia ihsani kubwa hii ya Allah. Kwa kuzikubali sifa hizi binadamu anapata shabaha ya kuumbwa kwake na kumuabudu Allah. Sheikh Amri anatangaza Tauhiid, na ukishampata Allah hapana shaka kila kitu kitaongezwa kwako.

Allah Ndiye pekee wa kusujudia. Na Sheikh Amri analiweka bayana hilo "Chini yako naanguka". Kwa nini mja asianguke ukifikiria fadhila zote ulizopewa, watoto, nyumba, akili, vyeo, umeya, mkuu wa mkoa, uwezo wa kutunga mashairi. Sababu kubwa ya yeye kuneemeka si nyingine ila mapenzi yake Allah. Kupitia kwake Amri anakiri "Kwako nimeneemeka". Na yote haya ni muujiza mkubwa kwa mtu aliyekuwa chini. Mwalimu Hassan anaeleza akifua kanzu usiku ili ikauke kwa upepo.

Sasa yupo katika hali ya ghanima. Na katika ubeti wa pili anaeleza sababu kwa nini muujiza huo umetokea. "Ni kwamba umeyataka waila yasingefika". Kupanda, kutakata, kunawiri hayo yote kwake ni "Kun faya Kun" - kuwa na inakuwa. Yote yanawezekana kwa ajili unapotaka. Hata wapige kelele, hata wakatae, hata wapinge, hata wavimbe mithili ya kisiwa cha Ukerewe, kitakachoshinda ni kudra ya Allah. "Kudra yake hutweka"

Mapenzi yote ya Sheikh Amri, raha yake, furaha yake, pumzi yake ni kukucha Mola wangu Wahadahu la Sharika. Jambo la pili linalompa sururi, linalompa buraha ni kuhudumu wenzangu kwa nia kuhalisika. Ni yeye kuwa mtumishi kwa kuwatumikia binadamu kwa



Gamal Abdul Nasser
Rais wa zamani wa Misri

upole, heshima na mapenzi . Neema hii ya kuwatumikia binadamu ni nzito. Waliopewa zaidi wataulizwa zaidi. Ni katika hali hiyo ndipo machozi humtoka na kumlilia Ghafura ili aendelee kukanyaga na kufuata njia iliyonyooka.

Sheikh Kaluta Amri Abedi ana elimu yakini dunia hii ni ya kupita. Tena ni mchezo na upuuzi. Tuko safarini. Tumepumzika tu kivulini. Tunasubiri safari ianze. Wazo ambalo Shabaan Robert analitilia mkazo;

Nambie vipi kufutu, mambo myazingatie
Hata aliye na kitu, haina mapenzi nae
Kama dunia si yetu, kwenda zetu tuandae

Kila ukishikacho duaniani hakidumu. Kinapukutika kama maua wakati wa kiangazi. Yanini kushughulika na ambacho kesho na keshokutwa kitakauka. Kufuata dunia ni kufuata majuto. Lakini nini imekuwa siri ya mafanikio yake? Kupanda kwake? Kutakata? Nini kimesababisha mabadiliko haya makubwa ya haraka? Anatusaidia katika kufichua siri ambayo haionekani kwa jicho la kawaida. Ni ubeti mzito;

Siri ya mafanikio, ambayo kwangu hutuka
Ni kwa dua za vilio, machozi kutiririka
Yakaumbwa matukio, na Mola Mwenye baraka
Kuvunja masingizio, na vijicho vya mahoka

Mafanikio yake yote kuzipanda hizi ngazi, kuneemeka huko kunatokana na ibada yenye khushui. Machozi hutiririka na isifikiriwe huu ni ubeti tu wa kufurahisha baraza la hasha! Sheikh Amri alikuwa anatokwa na machozi katika sala. Ushahidi tunaupata kutoka kwa mke wake Bi. Amina Mlenzi ambaye alishuhudia yote hayo. Sheikh Amri akilia mara nyingi kwenye sala hususan sala ya Tahajjudi. Hivyo kuelewa maisha ya Sheikh Kaluta Amri Abedi inatakiwa kufuatilia kwa karibu na kwa kisi gani alijitupa kwa Allah. Yeye aliamini ya kwamba hakuna mtu yoyote ambaye angeweza kumdhuru.

Kutokana na imani hii, hata umfanyie vitimbi hilo katu yeye hajali. "*Kwani ninaye Jalali nguzo ya kuegemeka*". Hivyo anatoa shuQur'an kwa Allah ambaye amempa neema, mafanikio na ulinzi. Anamuomba Amjalie hekima, Amuepushe na yote yaliyo mabaya. Anawataka na wengine wafuate njia hiyo ili waweze kufaidika na neema Anayotoa Allah. Anamuomba Mwenyezi Mungu siku yake ikifika; "*Dunia nikiihama nije kwa kuheshimika*". Sisi sote ni mashahidi kuwa maombi hayo yaliyotolewaCairoyalikubaliwa na Mwenyezi Mungu.

Bwana Mohamedi Saidi katika kitabu chake kuhusu AbdulWahid Sykes anakiri ya kwamba mazishi ya Sheikh Amri yalikuwa makubwa. Viongozi wa Afrika Mashariki na ya kati walikuwepo kwenye mazishi hayo. Ilitokezea ya kwamba wakati wa mazishi hayo viongozi hao walikuwa na mkutano wao hapa Mjini Dar es salaam. Jomo Kenyata wa Kenya, Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania, Milton Apolo Obote wa Uganda, Kiongozi wa Malawi Congress party Dr. Hastings Kamuzu Banda, Dr David Kenth Kaunda wa UNIP - Zambia. Mizinga 21 ilipigwa kwa heshima yake. Na ushahidi upi unaotakiwa kuhakikisha kuwa maombi hayo yalikubaliwa?

Kwa kumalizia shairi lake anatoa shuQur'an kwa Maliki Abdallah Mbungiro (Watachoka) ambaye amefanya kazi nzuri ya kumkumbusha kuwa asisahau mambo ya dini. Ni dhahiri kama alivyosema Seyidna Ali (ra) kwamba binadamu ni kiumbe wa ajabu sana, anakwenda makaburini anaona mtu anavyozikwa, anavyofukiwa, na akitoka hapo ameghafirika. Sheikh Amri anamshukuru Maliki Abdallah Mbungiro (Watachoka) kwa kumkumbusha na anamhakikishia ya kwamba atasauje mambo ya dini ambayo ndiyo yamemfikisha hapo alipo! Na akamhakikishia ya kwamba azidi kumuombea ili aweze kuendelea kushika kamba ya Mwenyezi Mungu.

Mwaka 1963 Sheikh Kaluta Amri Abedi alichaguliwa kuwa Waziri wa Sheria. Akimuapisha Rais Nyerere alimueleza ya kuwa changamoto kubwa kwake ni kusimamia harakati za kutafsiri sheria za nchi katika lugha ya kiswahili. Mara nyingi Mwalimu Nyerere alikuwa akisema kuwa anao wataalamu wawili wa lugha na wote ni kutoka Kigoma. Godwin Tunze ambaye alikuwa mtaalam wa lugha ya Kiingereza na Sheikh Kaluta Amri Abedi bingwa wa lugha ya Kiswahili.

Sheikh Kaluta alianza kazi hiyo kwa juhudi na bidii akawa anazitembelea nchi kadhaa kuona jitihada iliyokuwa ikifanywa katika uwanja wa kuwafanya watu waelewe sheria za nchi zao katika lugha zao. Moja ya nchi aliyoitembelea ilikuwa ni Misri. Sheikh alipata mapokezi mazuri na alifurahia kuwepo kwake Cairo kwani aliifahamu vilivyo lugha ya Kiarabu. Binti yake Bi. Radhia alinieleza kuwa Sheikh Amri alikuwa anapenda kusikiliza lugha ya Kiarabu na aliporudi kutoka Cairo alikuja na santuri zilizokuwa na mashairi mengi ya Kiarabu na alipenda kuzisikiliza.

Akiwa mgeni wa Serikali alikaribishwa katika hoteli ya kifahari inayotazamana na mto Nile. Upepo mwanana ulikuwa unavuma. Alisimama nje ya dirisha na kutizama mto Nile ulivyokuwa unatiririka kwa madaha kana kwamba hapakuwepo na jambo lolote jingine duniani. Alikumbuka mambo mengi ambayo mto huu ulikwisha yaona. Mateso ya wanaodhulumiwa na wale waliopata bahati ya kuonja raha. Katika kutizama kwake huko mtiririko wa mto ule roho yake haikuwa na utulivu hata kidogo. Hivi chimbuko la raha ni nini? Je nafsi inaweza kupata utulivu wa kutosha. Hizi tuitazo raha ni raha kweli? Mawazo makali yalianza na mgongano ukatokea kichwani. Kama maji yaliyokuwa yanatafuta mkondo wa kupita. Katika mahangaiko hayo ya kujibu maswali hayo yaliyokuwa yanamsumbua shairi zima lilikuwa tayari limekwishatulia kichwani. Alitafuta karatasi na kalamu na alipokaa chini ikatiririka mistari bila ya tabu ya kutafuta vina na mizani. Anasimulia ya kwamba hilo lilikuwa moja ya mashairi yaliyokuwa Sahari kwake kutunga. Mawazo yalitiririka kwenye karatasi. Shairi zuri hutoka vizuri unapokuwa umekabwa na mwiba wa maisha. Katika hali hiyo shairi linakuwa zito kama alivyowahi kushauri Sheikh Amri ukosapo neno jema heri kujinyamazia. Hivyo ndivyo lilivyozaliwa shairi lililochafua bahari ya ushairi kwa muda mrefu. Shairi hilo alilipa jina 'Raha'

Raha ya kweli kinaya, kukinahi yako hali
Ukaepuka mabaya, na mema ukayajali
Kisha usione maya, utosheke na akali
Ya upatacho halali, ndipo utaona raha

Ndipo utasalimika, ujapo miliki mali
Kwani hautazuzuka, wazuzukavyo juhali
Ambao huja umbuka, kwa zao mbaya amali
Na fedheha kuwadhili, katu wasione raha.

Na ukiwa masikini, huli vyema na hulali
Bali umtu amini, haramu huikubali
Hudhiliki abadani, mazito huwa sahali
Dhiki ukazihimili, mwisho ukaona raha

Si kila mara akwasi, ***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

Zawadi kwa Malkia Victoria

Kutoka uk. 1

Toka wakati huo alitumia wakati wake mwingi zaidi katika kutafakari juu ya maendeleo ya Ufalme wake.

Malkia Victoria alifanya kazi zake kwa uangalifu na akiwa na imani ya sera moja ya kwamba "TUNAWEZA" Dola lake likawa kubwa. Australia, New-Zealand, India, Africa na sehemu nyingi za Asia zikawa chini ya himaya yake. Hili lilikuwa ni dola lenye nguvu na viwanda kuliko mataifa yote ya wakati ule. Uingereza kwa hakika ilikuwa nafasi ambayo imeshikwa na Marekani hivi leo. Nguvu za kijeshi za Uingereza zilitokana na Wanajeshi wake wa majini ambao walionekana kuitisha dunia. Kwa busara zake kubwa Malkia Victoria aliepusha Uingireza isiingie katika vita vya Ufaransa na Prussia (Urusi ya sasa) mwaka 1870 - 1871. Kwa upande wa viwanda, viwanda vya Uingereza vilikuwa vinaongoza. Lanca Shire, Yorkshire, Burmingam, Sherbbid ni sehemu zilizozalisha vitu vingi na bora. London ndio ulikuwa mji wa mambo yanayohusu fedha na bima. Reli zilizojengwa Ulaya na Marekani zilipewa ufadhili na Uingereza. Maonyesho makubwa na maarufu ya 1857 yalikuwa ni uthibitisho wa hatua kubwa ya Uingereza katika viwanda. Viwanda nchini Uingereza viliota kama uyoga, na sehemu kubwa ya nchi hiyo iliunganishwa na reli.

Ni katika utawala wake ndipo walipojitokeza wavumbuzi maarufu akina Michael Faraday, aliyevumhbua mashine ya umeme. Charles Darwin aliyeandika juu ya mabadiliko ya binadamu. Mafundisho ya Darwin yalikwenda kinyume na mafundisho ya Biblia ambayo yalisisitiza kuwa binadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu. Licha ya kelele nyingi za kumlaumu Darwin, alipewa ulinzi na haki ya kueleza imani yake. Hii ni ishara ya utawala wa Malkia Victoria ulioruhusu tofauti ya fikra na rukhsa ya mtu kutoa fikra zake tena bila woga. Dhana hii ya uhuru wa mawazo ilifafanuliwa vizuri zaidi na John Stuart Mill, Thomas Macaulay, William Morris na Mathew Arnold ni wakati huu ndipo Uingereza ilipompata Malkia aliyekuwa anaongozwa na katiba.

Utawala wa Malkia Victoria ulishamiri na kutoa rutuba nzuri ya fikra na kwa njia hiyo kuweza kuzalisha miongoni mwa waandishi bora katika lugha ya Kiingereza. Ujuzi wa mtu haukamiliki hadi amewasoma hao magwiji walioandika wakati wa Malkia Victoria, Charles Dickens alichonga kalamu yake na kuishambulia jamii iliyokuwa inawatesa watu wa chini, riwaya zake *Blerk House*, *David copper field* na *Olver Twist* ni maarufu sana. Kalamu ya Dickens ilikuwa ni kali na sidhani viongozi wetu wangeliweza kustahamili ukali wa kalamu hiyo. Kama huamini muulize Ngugi wa Thiongo, Abdullatif Abdallah, Wole Soyinka, Chinua Achebe. Katika Uingereza ya Malkia Victoria walipewa heshima na kutambuliwa na jamii. Wengine ni pamoja na Emily Bronte aliyeandika *Wuthering Heights*, *Cholotte* aliyeandika *Jane Eyire* na Anne aliyeandika *Agness Grey*.

Mwaka 1867 serikali ya Uingereza ilitoa uhuru wa kupiga kura na vyama vya wafanyakazi vilipewa uhuru wa kutetea haki za wafanyakazi. Utumwa katika Afrika ulipigwa vita bila kujali sababu zilizowasukuma kuchukua hatua hiyo.

Huyu ndiye Malkia Victoria ambaye Masihi na Mahdi (as) alimpa hongera kwa sababu kiongozi mwema siku zote ni kivuli cha Mwenyezi Mungu. Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumia tukio hilo kumfikishia ujumbe mzito ambao ni kuacha kumuabudu kiumbe na kumuabudu Mwenyezi Mungu na kuwapokea manabii wote bila ya ubaguzi.

Sasa tunaingia katika kutizama maudhui ya vitabu hivi viwili "*Zawadi kwa Kaisari*" na *Nyota ya Kaisari*. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., mwanzoni tu mwa risala yake kwa Malkia anaweka bayana yeye ni nani. Ameeleza ya kwamba yeye amekuja katika kivuli cha Nabii Issa (as) hivyo yeye kama ilivyotarajiwa na wengi, yeye ni ujaji wa Nabii Issa (as) mara ya pili. Issa Mwana wa Mariyam alikwishafariki miaka mingi na kamwe hawezi kurudi duniani. Hivyo yeye ametumwa na Mwenyezi Mungu ili kuiachisha dunia bidaa za aina mbalimbali. Kusimamisha ukweli kwa njia ya amani na upole. Na baraka zote zinawafikia wale wanaompokea Nabii wa Mwenyezi Mungu.

Aliendelea kujenga hoja hiyo akimueleza Malkia kuwa Nabii wa uongo toka dunia ianze hajawahi kustawi na kupata maendeleo. Kila anayemzulia Mwenyezi Mungu anasagwa tikitiki. Kama hii ni kweli waanzilishi wote wa dini wametoka kwa Mwenyezi Mungu na wapo katika njia iliyonyooka. Kila watu Mwenyezi Mungu Amewatumia Nabii. Tunatakiwa kuwaheshimu na kuwakubali. Inatokea mafundisho mengine yanakwenda kinyume cha umoja wa Mwenyezi Mungu. Hii inatokana na ukweli ya kwamba mafunzo yanachafuliwa na mikono ya binadamu, kwani hayakupewa ahadi ya kuhifidhiwa. Ni Qur'an Tukufu pekee iliyopewa ahadi ya kulindwa. Fundisho hili la kuwaheshimu Manabii ni la msingi katika dini ya Islam. Ni dawa ya kuondoa machafuko na uhasama duniani. Mwenendo wa kukashifu viongozi wa dini ndiyo chimbuko la kuleta vurugu na tungewaheshimu viongozi wa dini machafuko lingekuwa ni katika mambo ambayo yangesahaulika. Na huu ndio uzuri na utamu wa Islam. Kabla maradhi hayajajitokeza tayari dawa imekwisha patikana. Inatakiwa mtu mwenye busara kumaizi ya kwamba maendeleo yote ya Jumuiyya ya Ahmadiyya ni ukweli na mwanzilishi wa Jumuiyya hii bila shaka ametoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hekima Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) anamwambia Malkia bila kumwambia "Mwenye macho haambiwi ona" na siku zote "Mti hujulikana kwa matunda yake" ni njia nzuri ilioje ya kumuita mtu kwenye haki. Kanuni hii ya kuwaheshimu viongozi wa dini ingefuatwa maeflu ya ufisadi na kashfa za kidini ambao ni kinyume cha amani baina ya watu kwa jumla zingetoweka. (Uk.10)

Dhana ya Jihadi katika istilahi ya dini ya Islam imeelezwa kwa weledi mkubwa. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ameonyesha ya kwamba jihadi inayo masharti yake, Waislam waliteseka sana Makka, ni wakati ule dhuluma ilipozidi ndipo Waislam walipigana vita vya kujihami na si kueneza dini. Islam inaelewa kuna dhana mbili za jihadi. Jihadi Saghir na Jihadi Kabir.

Vita kulazimika kupiganwa hiyo ni jihadi ndogo na jihadi ya kupigana na nafsi ili kutenda mema hiyo ndiyo jihadi kubwa. Hivyo hakuna funzo la kushika silaha katika Islam ili kueneza dini. Ni kosa zaidi kufikiri ya kuwa atakuja Masihi atakayeshika silaha na kuanza kumwaga damu. Masihi wa namna hiyo kamwe hatatokea. Serikali inayotoa uhuru wa kuabudu na kudumisha amani iantakiwa iheshimiwe.

Jambo kubwa ambalo Masihi Aliyeahidiwa (as) alitaka Malkia Victoria alizingatie na kulitolea maamuzi ni kwamba mafundisho ya Kikristo hivi leo hata Nabii Issa (as) akija leo hawezi kuyatambua. Ni dhuluma kubwa amefanyiwa ya kupewa sifa ya uungu. Hili ni chukizo kubwa sana. Na fikra ya kwamba Nabii (as) Mungu Apishe mbali alilaaniwa kwa sababu ya kufa msalabani hilo ni jambo ambalo hatuwezi kulikubali. Nabii Issa (as) alikuwa ni Nabii wa Mwenyezi Mungu na daima alifunikwa na kivuli cha cha mapenzi ya Allah. Ni kosa kudhani ya kuwa Nabii Issa (as) alifia msalabani. Mpendwa huyu wa Mwenyezi Mungu Alinusurika na kifo cha msalaba, akafunga safari hadi mashariki ya mbali na huko akakutana na kondoo wa Israeli waliopotea, akawafikishia ujumbe wake, akaoa, na kufariki akiwa na umri wa miaka 120 na kaburi lake linapatikana Srinagar, Kashmir India.

Masihi Aliyeahidiwa (as) alimshauri Malkia Victoria aachane na imani hiyo potofu. Kosa hilo lirekebishwe haraka sana. Na heshima ya Mpenzi huyo mwenye daraja la juu kwa Mwenyezi Mungu ihifadhiwe, kwa sababu katika lugha ya Kiarabu na Kiebrania neno laana lina maana ya kuwa mbali na Mungu na kumuasi. (Uk.36)

Tizama ujasiri wa simba huyu wa Mwenyezi Mungu anavyomuambia kwa hekima na mawaidha mema mkuu wa kanisa Malkia Victoria aachane na imani mbovu. Anamueleza huko aliko amepotea na dini ya kweli ni Islam. Kumwambia Mfalme / Malkia ukweli ni jihadi kubwa. Ni wangapi katiak miaka hiyo wangekuwa na ujasiri wa kumuambia Malkia aachane na imani yake? Ni dhuluma kubwa wanayomtuhumu Masihi Aliyeahidiwa (as) kuwa kibaraka wa Uingereza. Kama ukibaraka ni kumuambia Nabii Issa ni binadamu kama binadamu wengine si mtu ambaye amelaaniwa Mungu Apishe mbali, hakufa msalabani na wala hatakuja mara ya pili, basi ni afadhali ya ukibaraka huo kuliko kuamini ya kuwa Nabii Issa (as) yuko hai mbinguni wakati mbora wa viumbe wote sababu ya kuumbwa kwa dunia, rehema kwa walimwengu, siraju munir, Mtukufu wa daraja amezikwa ardhini.

Mara baada ya kutoa mwito kwa Malkia Victoria, Masihi Aliyeahidiwa (as) ameeleza shabaha ya dini tukufu ya Islam. Shabaha hizo ni mbili. Kwanza ni kumtambua Mungu Mmoja na kumuabudu na kusudi la pili ni kutumia nguvu zote kuwahudumia waja wa Mwenyezi Mungu kwa mapenzi na huruma kubwa.

Vitabu hivi viwili "Zawadi kwa Kaisari" na "Nyota ya Kaisari" ni mvua kutoka mbinguni kwa ajil ya wale wenye kiu ya kiroho na kurutubisha ardhi iliyo kame, kwani ukame huo unatokana na kuiacha Qur'an Tukufu.

بسم الله الرحمن الرحيم

TANGAZO LA IJITIMAA YA LAJNA NA NASIRAT 2013

Kwa Lajna na Nasiratul Ahmadiyya wote Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania.

Uongozi wa Lajna Imaillah Tanzania unawatangazia wana tanzeem wote kuwa, Ijtmaa yao kwa mwaka huu 2013 itafanyika Arusha mjini kuanzia tarehe 28 hadi 30 mwezi wa Juni 2013.

Wana tanzeem wote wanaombwa kujiandaa na kushiriki katika tukio hilo muhimu na pia kushiriki mashindano mbalimbali yatakayofanyika. Lajna na Nasirat wote wa kanda ya kaskazini na watakao toka mikoa mingine wajitahidi kufika Arusha jioni ya Alhamis ya tarehe 28/6/2013 kwa maandalizi muhimu.

Aidha kila Lajna na Nasirat anatakiwa ajiandae kwa mashindano mbalimbali kama tulivyokwisha wasiliana huko nyuma.

Limetolewa na:
Ofisi ya
Sadr Lajna Imaillah Tanzania

Mapango ya As-habul Kahf

Na Mwalimu Abdullah Khamisi Mbanga – Dar es salaam

Katika Sura Al-Kahf ya Qur'an Tukufu kuna simulizi za watu wa pango; watu ambao waliteswa kutokana na imani yao juu ya Mungu Mmoja na kuamua kufanya makimbilio katika mapango. Hawa bila shaka walikuwa ndio Wakristo halisi walioshikilia Tauhidi ambao imani yao ilikaribiana zaidi na Uyahudi kuliko Ukristo wa kisasa.

Katika Sura hiyohiyo ya Al-Kahf kuna maelezo yahusianayo na mahala yalipo mapango hayo kwa mwelekeo wa machweo na mawio ya jua. Kutokana na maelezo haya yapatikanayo katika aya ya 18 ya Sura hiyo inaweza kuwa rahisi kubainisha pango au kundi la mapango ambayo Qur'an tukufu inayazungumzia ambayo yalikaliwa na Wakristo hao wa mwanzo kwa jumla ya miaka 9 kati ya miaka 300 ya ukandamizwaji.

Katika makala hii tutaelezea ugunduzi mbalimbali wa mapango kwa mujibu mujibu wa taarifa za Wakristo na Wayahudi wa mwanzo na bila shaka huenda tukapata mwelekeo wa wapi Wakristo hao wa mwanzo waliishi.

MTAZAMO WA JUMLA

Historia ya mwanzo ya Ukristo inataja matumizi ya mapango na mahandaki kwa sababu maalum pale Ukristo ulipokuwa haujapata nguvu, kuzika wafu na mikutano ya siri. Mapango hayo wanahistoria huyaita 'Catacombs' kutokana na neno la kilatini Ad Catacumbas lililotumika katika ugunduzi wa mwanzo kabisa wa mapango ya aina hiyo nje kidogo ya jiji la Roma. Ukristo ulienea kwa kasi na upana zaidi katika maeneo ya utawala wa Kirumi kutokana na miundombinu, hivyo haishangazi kabisa kuona kuwa Wakristo wakikandamizwa na watawala wenye mashaka wa dola ya Kirumi.

Bila shaka historia inatupa taarifa kuhusu ukandamizaji uliofanywa chini ya Mfalme Nero mnamo mwaka 70AD, Mfalme Decius mwaka 249 – 251 AD na chini ya Valerian mnamo mwaka 257 – 258AD. Hatimaye, Constantine alitoa hati ya maridhiano ya Milan mwaka 313 AD na kuwapa Wakristo uhuru wa kuabudu.

Mapango kama hayo pia yamegunduliwa mnamo miaka 200 iliyopita katika maeneo mengine kadhaa ya Mediterrania. Mapango ya Qumran nay ale ya Nag Hammadi ambayo yalitumika kuhifadhia nyaraka na misahafu ya kanisa wakati wa ukandamizaji pia yatazingatiwa.

USHAHIDI WA MAPANGO YA KIYAHUDI

Kitabu cha kumbukumbu za historia ya Yuda 'Encyclopaedia Judaica' kinatoa taarifa kuwa mapango hayo yalikuwa ya Kiyahudi. Kinayaelezea mapango hayo kuwa ni yenye tabaka kadhaa za vijia vinavyoungana na vyumba vya maziko na baadhi ya makaburi yamejengewa katika kuta za vijia hivyo vijulikanavyo kama Loculi. Inasemwa kwamba mapango sita yaliyoko Rome ni ya Kiyahudi, nayo ni; Monteverde, Vigna Randanini, Vigna Cimarra, Via Labicana, Via appia pignatelli na Via Torlonia.

Tofauti kuu baina ya mapango ya Kiyahudi nay a Kikristo mbali na ile ya kisanaa, ni kwamba mapango ya Kikristo yana vyumba vikubwa vya mikutano ilihali yale ya Kiyahudi hayana. Hii ni kwa sababu Uyahudi enzi hizo tayari ilikuwa ni dini iliyoruhusiwa katika Dola ya Kirumi na hivi hawakuwa na sababu ya kuabudu kwa kificho.

Vile vile inaelezwa kuwa Wayahudi hawakupendezwa na desturi za wapagani katika maziko na hivyo waliamua kufanya shughuli zao za maziko kwa siri. Encyclopaedia hiyo inataja ni kuwa maandishi yaliyo katika makaburi mapangoni humo, yanayokadiriwa kuandikwa kati ya karne ya 1 hadi 4 AD kuwa 76% ni ya kigiriki, 23% Kilatini na maneno machache ya Kiebrania. Majina ya marehemu hao kwa kiasi kikubwa ni ya kigeni 46% Kigiriki, 31% Kilatini na ni asilimia 13 tu ndiyo ya Kiebrania. (Encyclopaedia Judica, Vol.5 Uk.249 – 252).

Ikiwa Uyahudi uliruhusiwa huko Rome, na tunaelewa kuwa Wayahudi walikuwa na viwanja vyao vya kuzikia, basi ni udhuru dhiafu sana kwao kuchimba mapango ya kuzikia kwa sababu tu eti ya kukwepa mila za maziko za kipagani. Mila za aina hiyo zilikuwa maarufu maeneo yote katika Dola ya Rumi na si katika mji wa Rome tu. Linaloshangaza zaidi ni kwamba ingawa Warumi walikuwa wakiishi Rome kwa karne nyingi, lakini haikuwa ila hadi baada ya ujio wa Yesu ndipo walipoanza kukerwa na desturi za maziko ya kipagani. Pia inashangaza kuona kwamba jamii inayothamini mno katika kutunza dini na utamaduni wake kama ilivyo kwa Wayahudi, ingeweza kutumia lugha za kigeni katika vibao vya makaburi yake na kwamba asilimia 13 tu ya majina hayo ndiyo yaandikwe kwa Kiebrania. Ingeingia zaidi akilini iwapo mapango haya yangekuwa ya Wakristo wa Kiisraeli, ambao walikuwa wakikandamizwa na Dola, na Waisraeli wenzao kwa ajili ya kumpokea Masihi wao, na walinyanyaswa hata na Wakristo wenzao wasiokuwa Waisraeli kutokana na kushikilia kwao sheria za Mussa na kudumisha baadhi ya desturi za Kiebrania. Kwa kuwa watu wa mataifa



Mwl. Abdallah Mbanga

waliishajiunga na dini yao, taratibu wangeweza kupoteza majina yao ya Kiebrania na kubakiwa na maeneo machache tu kwa ajili ya mambo muhimu ya kidini.

Ushahidi huu unaonyesha kuwa mapango haya ya Rome yumkini yalikuwa ni ya Wakristo wahafidhina ambao waliamini juu ya umoja wa Mungu, Unabii wa Yesu na walidumu katika sheria za Torati. Hoja hii inapata nguvu zaidi kutokana na kupatikana kwa baadhi ya nembo za nyenzo za kidini katika mapango hayo kama vile menorah (mshikio wa mishumaa wenye matawi saba), Sefer Torah (tawi la mtende) Shofar (kisu cha kutahiria) n.k. Vitu hivi vilitumika kwa Wayahudi na Wakristo zinaweka wakati huo kuwa ni kuanzia karne ya 3 na kuendelea.

Taarifa hizi zinaacha maswali mengi yasiyojibika juu ya umuhimu wa mapango hayo. Ikiwa hayakutumika kama makimbilio nyakati za mateso, ilikuwaje basi watu hao wajikalifu katika kuyaandaa? Encyclopedia ya mwanzo kabisa ya Katoliki inatoa picha tofauti kabisa kwa kurai kuwa Ukristo ulikuwa ukihesabika kuwa kama mojawapo ya madhehebu za Kiyahudi hadi mwaka 70AD, na kwa hiyo walizikwa pamoja na wananchi wenzao. Wayahudi waliyaendeleza mapango hayo hata kabla ya Wakristo kufika Rome, mapango hayo yalikuwa mfano wa makaburi – mawe ya kipalestiana ambayo ilikuwa ni katika mila zao.

Tofauti kubwa ya mapango ya Kikristo ni aina ya michoro iliyo maarufu katika Ukristo. Vilevile alama ya samaki huonekana katika baadhi ya maandishi kuanzia karne ya 3 na kuendelea.

Mapango hayo yamepakwa rangi zinazoonyesha picha za matukio kutoka Agano la kale na jipya, lakini michoro hii inasadikiwa kuwa ilianza kuchorwa kuanzia karne ya 4 na kuendelea.

Mwandishi J. Stevenson katika kitabu chake "The Catacombs-rediscovered monuments of early Christianity" anasema kuwa mapango yote ya Kikristo na Kiyahudi hayana tarehe ya kabla ya mwaka 150AD na kwamba hata yale mapango ya Kiyahudi si ya kale zaidi yaw a kale ambao walitahiriwa, walifuata suna zote za Torati ukiondoa zile bidaa za Mafarisayo.

USHAHIDI WA MAPANGO YA KIKRISTO

Kanisa Katoliki linaamini kuwa mapango ya Kikristo yanapatikana katika maeneo ya Rome, Naples, Syracuse, Malta na Tunisia. Wakristo wa mwanzo huenda walitumia maeneo ya makaburi ya wapagani lakini polepole walipopata nguvu na kumiliki maeneo ndipo wakaasisi maeneo yao ya makaburi.

Katika wakati ule suala la maziko lilikuwa ni ibada maarufu hasa miongoni mwa watu masikini. Inaaminika kuwa mapango ya mwanzo kabisa yanakadiriwa kuanza kutumika mnamo karne ya tatu ya Kikristo kama eneo la m aziko, mapango hayo inasemwa kuwa yalifunikwa na ardhi, lakini bado ndani ya mapango hayo kuna vyumba vya wazi hata sasa.

Baadhi ya makaburi yana maelezo binafsi ya watu waliozikwa. Hata hivyo kuhusu matumizi ya mapango hayo kama sehemu ya mikutano ya siri Catholic Encyclopedia inasema; "Hakuna ushahidi wowote wa ujenzi au matumizi ya mapango kama makimbilio nyakati za ukandamizwaji".

Halikadhalika mapango hayo yalinyang'anywa kutoka katika Kanisa katika wakati wa mateso, lakini yalirudishwa kwa Kanisa na Constantine. Pia anaonyesha kwamba vyumba Fulani bila shaka vilitumika kama vituo vya kuwaunganisha upya Wakristo. Pia ni jambo la kushangaza kwamba katika sanaa za michoro zilizomo katika mapango hayo, "Mateso, Kifo, Ufufuo na kupaa kwa Yesu sii mambo yaliyozingatiwa na hayana mvuto wowote".

Kwa kuwa mambo haya ndiyo msingi mkuu wa Ukristo, na kwa kuwa kazi za sanaa katika mapango hayo zinaonyesha matukio mengi ya Biblia, huu ni ushahidi wa wazi kuwa Ukristo wa sasa unaoegemea juu ya kafara ya Yesu ni imani ngeni kwa Wakristo wa kale. Tena jambo hili linaonyesha kuwa huenda watu wa pango walikuwa Waumini wa TAUHIDI na kamwe hawakuwa na dhana yoyote juu ya uana wa Mungu wa Yesu, kifo cha msalaba na ufufuko. Maoni haya bila shaka ndio msimamo wa Qur'an Tukufu Sura Al-Kahf.

MAPANGO NJE YA ROME

Kama ilivyo tajwa mwanzoni, mapango pia yamewahi kugunduliwa katika Mediterranean, Afrika Magharibi na Syria. Kuna mapango sita katika mji wa Naples kwenye eneo la Capodimonte. Yale ya San Gennaro yanakadiriwa kuwa ni ya karne ya 4AD na yana tabaka mbili. Yaliendelea kutumika kwa muda mrefu zaidi kuliko yale ya Rome na haya yalitumika wakati wa maambukizi ya Tauni. Mapango haya yana vichochoro vipana na kumbi kubwa kubwa za kuchongwa na sehemu za ibada zilizochongwa katika mawe magumu mno. Mapango hayo yalinakishiwa kwa rangi, nakishi zake zilionekana kutohusiana kabisa na Ukristo wa leo. Nakishi hizo zimezibwa kwa kupigwa lipu.

Juu ya sicily kuna maeneo 23 ya Wakristo, yakiwamo mapango yaliyoko Syracuse na Catania. Sarafu zilizopatikana humo zinaashiria kwamba mapango hayo yalitumika tangu karne ya 3 AD. Ingawa mapango haya yanafikiriwa kuwa yalitokea katika umiliki wa wapagani na kuhamia kwa Wakristo, lakini inaaminika pia kwamba katika kisiwa hiki kulikuwako na mapango mengi ya Wayahudi. Ishara kubwa ni kupatikana kwa menorah ya kuwekea mishumaa wakati wa ibada.

Katika mji wa Sousse huko Tunisia mapango matatu ya Wakristo yaligunduliwa yakiwa pamoja na pango dogo la wapagani. Eneo hilo inasemekana lilitumika kutoka mwaka 230 hadi karne ya 4 AD, na Ukristo unajulikana kuwa ulikuwa na nguvu katika eneo hili la dunia kunako karne ya pili. Kwa ujumla kuna takribani makaburi 1300, lakini vijia vyake ni vidogo mno kuliko sehemu yoyote.

Katika nchi ya Malta pia kuligunduliwa mapango ya Wakristo na Wayahudi ambayo yalifanana mno na makaburi zama za kabla ya Ukristo. Sifa moja ya mapango hayo ni kuwapo na meza ya duara ya Agape sakafuni, ambayo bila shaka ilitumika katika karamu za chakula za kuwakumbuka mashahidi.

Hatimaye kuna mapango mengine yaliyogunduliwa katika maeneo ya Libya, Alexandiria huko Misri na eneo linguine lijulikanalo kama Necropolis karibu na mfereji wa Canopus ambapo vijia vyake vina mpangilio maalum kuliko ile ya Rome, pia kuna mapango katika eneo la Emesa huko Syria ingawa kuna uhaba mkubwa wa taarifa kuhusu mapango hayo katika maandiko ya watafiti wa kadhia hii.

MAPANGO YA QUMRAN

Mapango ya Qumran yanapatikana kwenye maeneo ya miinuko katika Wadi Qumran, kwenye ukanda wa bahari ya chumvi. Yaligunduliwa mwaka 1947, na humo kuligunduliwa miswada ya maandiko iliyokuwa imefungwa katika vitambaa, m iswada hiyo ni maarufu kwa jina la Dead Sea Scrolls iligunduliwa ikiwa imefunikwa na lundo kubwa la mawe kwa kusudi la kuhifadhiwa.

Mapango haya yapo karibu sana na Khirbet Qumran monastery nyumba ya watawa

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Bustani ya Washairi

Mashairi ya Kiswahili yana utamu wake. Na mengi ya mashairi hayo yanakumbukwa kwa ghaibu. Moja ya shairi maarufu la Kiswahili ni hili lililotungwa na Hamadi Magambo (Msanifu) wa Kilosa. Ingawaje shairi hilo limetungwa mwaka 1945, maudhui ya shairi hilo yanagusa ukweli wa maisha yetu ya hivi sasa.

1. Limbukeni hana siri, hawezi kujizuia
vigumu kujisitiri, kuchunga wake murua
jambo lenye taka siri, enda akalisifia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

2. Hana budi kujisifu, huku akijifutua
kujiona ni nadhifu, na mwerevu wa kujua
wenzie huwakashifu, kisha akiwaumbua
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

3. Halisikii la mtu, japo wakimuambia
huwafanya ni viatu, au la pundamilia
matusi kwake si kitu, kuwavunjia tabia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

4. Kujifanya ni mjuvi, kila jambo kumwelea
haheshimu wenye mvi, wala aliyemlea
ndugu kwake huwa mwivi, wala hataki mwendea
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

5. Anapoipata mali, izidipo penye mia
hapo huona muhali, ugali kuutumia
hutaraji kula wali, kwa manyama ya ngamia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

6. Hayamwishi majivuno, lau ukimwamkia
zapita dakika tano, ndipo kukuitikia
sijaona kwa mfano, wala kupata sikia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

7. Moyo ukitaazizi, hali ukimshtakia
kukuona mpuuzi, na hadhi kukuvunjia
tazameni huyu mwizi, kaja kutaka nibia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

8. Ulizidisha shauko, vingi kukukatalia
hataki chai mkoko, japo akiitumia
huzikashifu choroko, zinacho kiungulia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

9. Mwaka mmoja hamalizi, mali imempotea
imebaki simulizi, heshi kutuhadithia
sinione siku hizi, zamani nikitishia
kila anaelimbuka, kujisfu hana budi.

10. Mpanda ngazi hushuka, acheni wenu udhia
wangapi walozishika, wenye sifa kuzidia
sasa wanahangaika, zote zimewakimbia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

11. Kweli watu walisema, mali pambo la dunia
bali itumie vyema, sibadili yako nia
uwatunze mayatima, nao wapate timia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

12. Kaditama ni yakini, abishae tamwambia
Mahamudu Hamduni, sema yaliyobakia
niko kilosa mjini, zana nimekwisha pakia
kila anaelimbuka, kujisifu hana budi.

Katika bustani ya washairi, tuliwahi kujenga hoja ya kwamba Julius Kambarage Nyerere ni mshairi wa sifa. Mmoja ya wasomaji wetu alitaka ushahidi. Tunawaletea moja ya shairi lake.

1. Watu ni sawa nasema, zingatia neno watu
siwapimi kwa vilema, ambao ni udhia tu
siwafanidi kwa wema, ambao ni tabia tu
lakini watu ni watu, mawalii nawagema.

2. Niseme maji ni maji, pengine utaelewa
yakunywa na mfereji, na yanayo ogelewa
ya umande na theluji, na mvua mito maziwa
asili yake ni hewa, hayapitani umaji.

3. Yatie chumvi na mvua, hayaachi kuwa maji
safi ukiyachafua, utakera tu wanywaji
yapashe moto kwa jua, hayaongezi umaji
maji yeyote ni maji, maji nusu wayajua?

4. Binadamu kadhalika, wote kabisa ni sawa
si kwa nywele au rika, au wema na utawa
au huyu kusifika, yule kudharaulika
ni wanadamu na hawa, asili ya kuumbika.

5. Wala si kwa asili tu, ni sawa kwa thamani
tajiri mwingi wa vitu, ukimuua hayawani
madhari wote ni watu, hataachwa duniani
sawa ya mtu ni nini? Sawa ya mtu ni mtu.

6. Sijakana nakubali, unanizidi kwa kimo
tena mwingi wa akili, mwenzio mimi hazimo
bandani wewe hulali, nyumba yangu mimi shimo
japo niwe mbilikimo, sote tu watu kamili.

7. Anzali na bwana Jaji, Mkuu wa mahakimu
wayavina watungaji, na wote wenye elimu

maskini waombaji, na wanaowa karimu
wote ni binaadamu, watunzi na wasomaji.

8. Kimo hanizidi twiga, kimo wakitajiani?
Kina tembo twawapiga, wahodhi mali puani
Elimu ni ya kuiga, waiga hata manyani
Lakini nyani ni nyani, hawi mtu kwa kuiga.

9. Tukiri una mwandani, mwanana mzuri sana
hana doa asilani, anae wa kulingana
mambo hayajulikani, kesho awe pua hana
mwandani utamkana, kuwa sasa si mwandani?

10. Ulozi si jambo jema, si kani kamwe sikani.
Ila mlozi nasema, ni mtu siye shetani
Na walii mtu mwema, ni sawa na malu'uni
Umtu hawapitani, mtu mbaya na mwema

11. Usawa wa binadamu, si usawa wa sarafu
hata sarafu fahamu, kuna safi kuna chafu
bila bibi bila amu, sawa bila hitilafu
usawao nakuarifu, ni wao ubinadamu.

Miaka zaidi ya mia moja iliyopita, Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (AS) alielezwa na Mwenyezi Mungu ya kwamba Nabii Issa (AS) amekufa. Tangazo hilo la kifo cha Nabii Issa (AS) lilizua balaa. Kitabu cha Masihi Aliyeahidiwa kiitwacho Yesu katika India, siyo tu kimeeleza ya kwamba Nabii Issa amefariki, bali kaburi lake limeonyeshwa na ukoo wake umetajwa. Katika shairi hili, Sheikh Kaluta Amri Abedi amewapa pole mapadre kwa msiba huo na tunadhani pia baadhi ya Masheikh wanahusika na msiba huo nao tunawapa pole. Inna lilallahi wainnaillahi raju'un.

1. Afile nabii Issa, Nabii Issa afile
kinyume cha hilo kosa, la kanisa tangu kale
wacheni mambo ya visa, Qur'an msomele
Yesu kalala afile, poleni mabwana padili.

2. Hakufa msalabani zilifunga pumzile
akazinduka pangoni, alimotiwa alale
akatoroka mjini, akaenda Galilele
Yesu kalala afile, poleni mabwana padili.

3. Alifika Kashimiri, akafia kulekule
mtaa wa Khaniyari, ndipo kwenye kaburile
matanga yawasubiri, fikeni kule mlole
Yesu kalala afile, poleni mabwana padili.

4. Tunawahani makiwa, mabwana padili pole
siri zimefichuliwa, Mungu wenu alifile
winguni hakuchukuliwa, wacheni ndaro za kale
Yesu kalala afile, poleni mabwana padili.

5. Mungu wetu ni Jalali, wa tangu na wa milele
Hafi hasinzii hali, hazaliwi hana ndwele
Ni yeye Mungu wa kweli, vipi mwapotea vile
Yesu kalala afile, poleni mabwana padili.

DUA

1. Bismillah hakika, Mola wangu ninakuja
Wewe uso mshirika, ni kwako najikongoja
Dua kwako ikifika, hakuna mtia hoja
Ninawaombea dua, khuddam wa Tanzania.

2. Dua kwako ikifika, hakuna mtia hoja
Ninakuomba Rabuka, tuzidishie umoja
Katu tusije anguka, kwenye dimbwi la viroja
Ninawaombea dua, khuddam wa Tanzania

3. Katu tusije anguka, kwenye dimbwi la viroja
Khuddam wanasifika, kwa kazi ni namba moja
Kweli wameimarika, wengi twapata faraja
Ninawaombea dua, khuddam wa Tanzania

4. Kweli wameimarika, wengi twapata faraja
Mambo yao kupangika, wametupa mkongoja
Tabora hadi Mangaka, khuddam tupo pamoja
Ninawaombea dua, khuddam wa Tanzania

5. Tabora hadi Mangaka, khuddam tupo pamoja
Beti tano zimefika, salamu kule Unguja
Kwa Mola zake baraka, ipo siku nitakuja
Ninawaombea dua, khuddam wa Tanzania.

Pazi Mazongera (Kiumbe Mzito)
Masanganya-Chamgohi.
Kisarawe.

BINADAMU NI DHAIFU

1. Usaghiri ja siafu, ya nini hayo maringo?
Humanyi wewe dhaifu, toka siha na ubongo?
Hatimayo kutawafu, kuzikwa kwenye udongo?
Binadamu ni dhaifu, tena ni dhaifu sana

2. Nisemayo ashirafu, usambe ni masimango
Majuto huja halafu, hususan kwa msungo
Wako wapi maarufu, walotisha kwa maungo?
Binadamu ni dhaifu, tena ni dhaifu sana

3. Siru na huku wahofu, dunia ni kikaango
Hukugeuza mnofu, wa bakara na kononngo
Wako wapi watukufu, wa Pate na wa Mkongo?
Binadamu ni dhaifu, tena ni dhaifu sana

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MANDHARI YA MWISHO

Afya ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. ilianza kuharibika mwanzoni mwa Januari 1914. Alihisi maumivu katika mbavu, mara kwa mara alipata homa na kichefuchefu. Akaanza kudhoofika, lakini alikuwa mchangamfu na akaendelea kutoa darasa la Qur'an Tukufu kila siku. Alipoona shida kupanda ngazi za Masjid Aqsa, akatoa darasa katika uwanja wa Madrasa Ahmadiyya, lakini alitakiwa kusaidiwa kutembea umbali kidogo hadi Madrasa, kwenda na kurudi. Udhaifu wake ukazidi na darasa likahamishwa katika chumba kimoja katika nyumba ya mwanaye mkubwa, iliyo jirani na nyumba yake mwenyewe, na akatoa darasa akiketi. Madaktari wake wakamshauri kuacha kutoa darasa, lakini akakazania kwamba maadamu anaweza kusema, hana budi kuendelea kufafanua Neno la Mungu.

Mwanzoni mwa Februari ikafikiriwa ya kwamba yeye anaugua kifua kikuu. Dkt. Mirza Yakub Beig akawasili kutoka Lahore na pamoja na Dkt. Khalifa Rashiduddin akajitolea kumwangalia mgonjwa mtukufu ambaye kidogo kidogo akawa dhaifu, sauti yake ikawa ndogo, akala chakula kidogo sana. Tarehe 14 Februari, Col. Melville akatumwa kutoka Lahore. Akawasili pamoja na Dkt. Seyyid Muhammad Husain na akamchunguza kikamilifu, matokeo yake akahakikisha usawa wa uchunguzi wa madaktari waliokuwa wakimtibu, akakubali dawa waliyotoa na akapendekeza chakula kiongezwe. Baada ya yeye kuondoka, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akanena:

"Daktari kutoka Lahore alichukua muda mwingi kunichunguza. Ugonjwa ninaougua ni rahisi sana kuchunguzwa kiasi hiki kwamba ninaposhughulika katika zahanati yangu na mtu anapoingia mlangoni na kuniamkia, mimi natambua kwa sauti yake pasipo kumtazama kwamba anaugua maradhi haya."

Kwa kuona udhaifu wake unaendelea kuzidi, madaktari wake wakaamua kwamba ahamishiwe kwenye nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a., iliyokuwa katika bustani kubwa nje ya mji na ambako atakuwa na raha zaidi. Nawab Sahib alipenda sana kumkaribisha na mara mbili akamwomba pia. Hatimaye akatoa kibali chake na akahamia huko mnamo Februari 26.

Mwanzoni mwa Machi, Dkt. Seyyid Muhammad Husain alimtembelea Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., na katika maongezi akasisitiza uzuri wa kushirikiana na madhehabu mbalimbali ya Waislamu kutafuta shabaha zilizo sawa baina yetu; hapo Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akasema:

"Tumeweka mfano wa ushirikiano wa aina hii kuhusu habari ya kuanzisha Chuo Kikuu cha Waislamu. Ushirikiano wa aina hii unafaa, lakini ni muhimu kabisa kudumisha umoja wetu wazi wazi. Maendeleo huongezeka kwa sababu ya kupambanuka. Kuchangamana kwa jumla huharibu nguvu ya kuchukua hatua na kuzuia maendeleo. Tena hatuwezi kujiweka chini ya waliokataa Mwanzilishi wetu aliyetumwa na Mungu. Na kipambanuzi kisipodumishwa, kuamrisha mema na kukataza maovu hakuwezi kutunzwa. Kundi moja linapopambanuka, upinzani hupatikana; na jinsi upinzani unavyozidi, wale waliopambanuka hukimbilia kuomba dua na kutia bidii nyingi zaidi. Shida huhimiza kutia bidii, kujitahidi na kufanya maombi. Mtu anayeafikiana na kila kitu hafaulu kupata kitu."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaandika wasia wake kwa mkono wake mwenyewe mnamo Machi 4, ambao ni huu ufuatao:

"Kwa jina la Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

Twamhimidia Yeye na kumsalia Mjumbe Wake Mtukufu.

Mnyenyekevu huyu, akiwa mwenye akili timamu, anahakikisha: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu; Muhammad s.a.w. ni Mjumbe wa Mungu. Watoto wangu bado ni wadogo, nami sina mali. Mungu Atawahami. Wasipewe kutoka katika mfuko wa mayatima ama maskini. Waweza kupatiwa karadha njema itakayolipwa na baadhi ya wanangu wenye uwezo. Vitabu vyangu na milki yangu ifanywe Trust (Amana) kuwanufaisha watoto wangu. *Khalifa* baada yangu awe yule aliye mwema, apendwaye na watu, mtaalamu na mwenye mienendo mizuri. Asamehe makosa na awavumilie marafiki wa zamani na wapya wa Hadhrat Sahib a.s. Jinsi nilivyokuwa mwenye kuwatakia heri wote, ndivyo anavyotakiwa kuwa yeye. Darasa la Qur'an Tukufu na la Hadithi liendelee.

Wassalamu.

Nuruddin. Machi 4, 1914."

Akampa Maulawii Muhammad Ali wasia huo na kumwambia awasomee waliopo. Akaagiza kusomwa mara ya pili na mara ya tatu, kisha akauliza kama jambo lolote limebakia;



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

akajibu Maulawii Muhammad Ali kwamba huo ni sawasawa. Halafu akaukabidhi kwa Nawab Muhammad Ali Khan r.a. kuuhifadhi.

Udhaifu ulivyoendelea kuzidi wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. ukazusha fikira kwamba itakuwaje akifariki. Fikira hiyo ikafichua hitilafu kubwa zilizotoa ishara ya fitina na mafarakano. Katika hali hiyo Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad akaandika tangazo kwamba kueleza hitilafu ambapo Hadhrat Khalifatul Masihi angekuwa na afya njema isingeleta uharibifu mkubwa, kwani yeye angeweza kuizuia na kuiweza. Lakini sasa kwa kuwa yu mgonjwa sana, mabishano hayo yanaweza kusababisha taabu, kwa hiyo mabishano ya aina hii yaachwe kwa muda mpaka Mungu Amjaalie afya kamilifu. Mwandiko huo wa tangazo akampelekea Maulawii Muhammad Ali na akapendekeza kwamba hilo laweza kuchapishwa kwa sahihi za zote kwa pamoja. Lakini Bwana huyo akakinza na kusema kwamba njia nzuri itakuwa kuitisha kikao na sisi wawili tukihutubie namna tupendavyo. Basi kikao kikaitishwa katika Masjid Nur na Maulawii Muhammad Ali akamwomba Sahibzada Sahib kusema kwanza. Hapo yeye akaeleza aliyokuwa ameandika katika tangazo. Halafu Maulawii Muhammad Ali akazungumza, na akawakaripia vikali wale waliomlaumu Khwaja Kamaluddin na wenzake waliofikiria kama yeye. Akasikilizwa kwa kimya chenye uchungu. Mwishowe akaongeza maneno machache kwa sauti kali kuhusu haja ya kuwa na upatano. Hotuba yake ikazidisha udhia uliokuwapo mapema.

Sahibzada Sahib akaendelea kushughulikia maombi na dua, na akawahimiza marafiki zake kufanya hivyo. Yeye hakujali sana hitiliafu za rai kuliko kulinda umoja wa Jumuiya ambao aliuthamini zaidi sana. Akaongea na wanajumuiya wengi wenye kuathiri na akagundua kwamba waliokuwa na maoni ya kuwepo kwa *Ukhalifa* na wakauamini unabii wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. hawawezi kufanya baiati ya yule azipingaye itikadi hizo, kwani hiyo itamaanisha Uahmadiyya kukoma. Lakini akaamini kwamba umoja una thamani zaidi wala usitupiliwe mbali kwa ajili ya watu fulani. Akaanza kuwasisitizia marafiki zake ya kwamba kama baada ya kufariki Hadhrat Khalifatul Masihi ikitokea hatari ya mafarakano, wapaswa kujiweka tayari kufanya baiati ya mmojawapo wa kundi la watu wachache, kwani wao hawatamkubali asilani yule anayehitilafiana naye na Jumuiya itafarakana. Lakini yeye akifanya baiati ya mmojawapo kati ya hao, marafiki zake watafuata mfano wake na umoja wa Jumuiya utahifadhiwa. Jioni moja akatumia masaa mawili kumsisitizia Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a., Sheikh mmojawapo wa mstari wa mbele wa Jumuiya, kukubali maoni yake kwamba hitilafu ikitokea kuhusu nani awe *Khalifa*, watakuwa tayari kufanya baiati ya mmojawapo wa kundi la watu wachache. Ama kuhusu mambo ya hitilafu, ni hivi kwamba maadamu *Khalifa* hatoi maagizo kuhusu hayo, watakuwa na uhuru wa kufuata na kuendelea kuamini wanayofikiria ni sawa na kweli. Na kama *Khalifa* akitoa agizo kuyahusu hayo, watalazimika kumtii na kukaa kimya, wakimwachia Mungu swala hilo mkononi Mwake, Ambaye ndiye Mlinzi wa kweli wa Jumuiya.

Katika siku za mwisho za ugonjwa wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., Pir Iftikhar Ahmad r.a. akamwambia ya kwamba *Masufii* wanaamini kwamba maisha ya *Sufii* ni baraka kwa ajili yake mwenyewe na pia kwa wengineo, na akamsisitizia ajiombee kwa kupata afya. Akajibu: Nasikia daima: "Sivyo! Bali nyinyi mnapenda maisha ya sasa, na mnaacha maisha ya Akhera (75:21-22)." Hayo yalikumbusha majibu aliyotoa Hadhrat Abu Bakr r.a. kwa pendekezo la aina hiyo alipokuwa katika hali kama hiyo. Alisema: "Nimeomba na nimepokea jawabu: Najua vizuri zaidi. Nitafanya nitakavyopenda."

Kabla ya saa sita za mchana, siku ya ijumaa, Machi 13, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akamwita mwanaye mkubwa, Mian Abdul Hai na kumwambia:

"Siku zote nimeamini: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu, nami nafa nikiamini hiyo. Nawaheshimu masahaba wote wa Mtume Mtukufu s.a.w. Baada ya Qur'an Tukufu naona kitabu cha *Bukhari* cha Hadithi za Mtume s.a.w. chakubalika zaidi kwa Mungu. Namwamini Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mteule wa Mungu. Nilimpenda sana hata kwamba niliwapenda watoto wake zaidi kuliko wewe. Nakutupa kwa Mungu Mtukufu, nami nina yakini ya kwamba hatakuacha uangamie. Nakusihi kusoma Kitabu cha Mungu, kukifundisha na kutenda sawa nacho. Nimejionea vitu vingi sana, lakini sijaona kitu kama Qur'an. Pasipo shaka yoyote, hicho ni Kitabu Chake Mungu Mwenyewe. Kwa mengine nakuacha mkononi mwa Mungu."

Saa za sala ya Ijumaa zikawadia, na kwa kuacha wahudumu wawili au watatu, wengine wote wakaenda Masjid Aqsa kusali. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akafanya *Tayammamu* na kusali. Alipomaliza tu kusali, kupumua kukawa taabu na katika dakika chache roho yake ikaaga mwili wake dhaifu kwenda kupumzika milele. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Habari hii ya msiba mkubwa ilipofika msikitini, Masjid Aqsa, ambapo sala ya Ijumaa iliyokuwa inaongozwa na Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad ilikwisha tu, kila mmoja akakimbilia nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a. ili kuona uso uliopendwa wa yule ambaye kila dakika yake ilikuwa imetolewa wakfu kusogeza mbele miradi ya ustawi wa kiroho na wa kimwili. Kwa hiyo watu wengi sana wakashiriki katika sala ya alasiri katika Masjid Nur, msikiti uliokuwa karibu zaidi na nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a. Baada ya sala, Sahibzada Mriza Mahmud Ahmad r.a. akawahutubia kama ifuatavyo:

"Sawa na matakwa ya Mungu, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. amefariki. Mungu Amrehemu na kumbariki sana, na kumnyanyua kwenye madaraja ya juu kabisa na kumwunganisha na Mtume Mtukufu s.a.w. na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambao alijitolea kwao na kujaa mapenzi yao.

Sasa wanajumuiya wa Jumuiya Ahmadiyya wana wajibu mzito sana. Jumuiya nzima inakabili jaribio. Yule atakayefaulu katika mtihani huu atajinyakulia kibali na huba ya Mungu; na atakayefeli katika mtihani huu hatahesabiwa mwema mbele yake. Hatuna budi kujitayarisha kikamilifu kupita katika mtihani huu. Zingatieni vizuri kwamba mpango mzuri kabisa hugeuka kuwa chanzo cha hatari ikiwa nia inayouongoza si safi. Sala ndiyo njia njema mno ya kupata usafi, hata hivyo ikanenwa:

Endelea uk. 8

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Kutoka uk. 7

'Basi ole kwa wanaosali, ambao wanapuuza sala zao, ambao hufanya ili waonwe" (107:5-7). Hivyo, sala iliyoongozwa na nia mbovu haiwi njia ya kupata usafi na ukaribu wa Mungu, bali huwa laana.

Twasihiwa kutafuta kinga ya Mungu dhidi ya Shetani kabla ya kusoma Qur'an Tukufu, na kila sura inaanza kwa Jina la Mungu, na hii ndiyo njia ya kupata msaada wa Mungu. Hili ni dokezo ya kwamba kabla ya kuanza jambo zuri kabisa kama usomaji wa Qur'an Tukufu, mtu hana budi kujikinga kwa Mungu katika shaka na wasiwasi wa Shetani, na kutafuta msaada wa Mungu ili kujaaliwa uwezo na nguvu ya kutekeleza kazi kubwa ya usomaji wa Qur'an. Watu wengi hupata rehema ya Mungu na baraka Zake kutokana na aya moja pekee ya Qur'an Tukufu, na aya hiyo hiyo yawa chanzo cha maangamio kwa wengi. Ndiyo sababu imeamriwa kujikinga kwa Mungu. Kwa kifupi, mpango hata ukiwa mzuri namna gani, lakini kama haukupendekezwa kwa uaminifu na nia safi, kuna hatari ya kwamba mpango huu utapeleka mbali na Mungu.



Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. - Mtunzi wa kitabu hiki

Hatuwezi kutekeleza wajibu mzito tuliotwishwa saa hizi pasipo rehema ya Mungu na kujaaliwa uwezo naye. Hivyo, nawasihi kutumia wakati wote mlio nao katika kuomba: E Mola, Tuongoze njia ya haki ili tulindwe katika maangamio na tukusogelee karibu zaidi. Huu ni wajibu mkubwa usioweza kutekelezwa bila msaada wa Mungu. Kazanieni dua hii: Utuongoze njia iliyonyoka (1:6). Hatuelewi itabainika nini kesho au kesho kutwa. Yote hiyo imefichikana tumboni mwa wakati ujao, nasi tusipoongozwa na kusaidiwa na Mjuzi wa mambo ya ghaibu tutajitia katika hatari ya kuangamia. Kwa hiyo, ombeni dua, ombeni kusamehewa na kukingwa dhidi ya kufanya kosa, ombeni kuongozwa na kumsalia Mtume Mtukufu s.a.w. Ombeni kwa uchungu: Mola, tusaidie kupita katika mtihani huu kwa huruma Yako. Masihi Wako alitokea, na wengi wakamkana na wakajikwaa na kuanguka juu ya mwamba huo na kujiangamiza; lakini wewe Ukatuongoza kwa huruma Yako. Alipofariki tukakabili jaribio, nawe Ukatuongoza tena. Sasa twakabili jaribio mara nyingine. Utujaalie tena rehema Yako na Utuongoze, na Ututilie baraka katika mambo yetu, wala Usiwafanye maadui zetu kufurahia kushindwa kwetu, na Umchague mtukufu kati yetu kwa huduma Yako. Amin.

Kila mmoja ashughulikie maombi wakati wote. Amkeni usiku kumuomba Mungu. Mungu Hutatua matatizo yote kwa rehema Yake. Mtegemeeni Mungu. Ahadi Zake zote ni za kweli. Ahadi Alizomwahidi Masihi Aliyeahidiwa zimetimia na zinaendelea kutimia. Binadamu aweza kufanya ahadi ya uwongo, lakini ahadi za Mungu ni za haki, naye Yu Mwaminifu kwa ahadi Zake. Mwalazimika kumtawakali na kumtegemea Yeye. Sasa nitaomba, nanyi mwungane nami katika maombi yangu, na halafu mwendelee na maombi yenu."

Akainua mikono yake kwa maombi ya kimya, na wote

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

بسم الله الرحمن الرحيم

TANGAZO LA IJITIMAA YA KHUDDAM NA ATFAL

Kwa Khuddamul Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya wote Tanzania.

TANGAZO LA IJTMAA YA 24 YA MWAKA 2013.

Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inawatangazia wana tanzeem wote kuwa, Ijtmaa ya 24 itafanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 21 hadi 23 mwezi wa 6 katika viunga vya Jumuiya Ahmadiyya Kitonga. Wana tanzeem wote tunaombwa kujiandaa na kushiriki katika tukio hilo muhimu na kushiriki mashindano mbalimbali yatakayofanyika. Watu wote na watakao toka mikoani wajitahidi kuwa kitonga kabla ya sala ya Ijumaa ya tarehe 21 kwa maandalizi muhimu. Aina ya mashindano yatakayofanyika yanahitaji maandalizi na yatakuwa kama ifuatavyo:

MASHINDANO YA ELIMU YA DINI IJTIMAI YA KHUDDAM 2013

KHUDDAM	*ATFAL*
HIFDH QUR'AN Mashindano matatu 1. Juzuu 30 (A'ama) 2. Juzuu 29 na 30 3. Juzuu 30, 29 ,28 na 27	**HIFDH QUR'AN** Mashindano matatu 1. Juzuu 30 (A'ama) 2. Juzuu 29 & 30 3. Juzuu 30, 29, 28 na 27
TAFSIRI YA QUR'AN 1. Sura Al-hujuraat (49) Aya 1-6 2. Sura Al-Jumu'a (62) Aya 1-9 3. Sura Al-Fat'h (48) Aya 28-30	**SALA YA KIISLAM** Umri wa chini ya miaka 10. 1. Adhana 2. Kukimu sala 3. Adhana ya Alfajiri Kuanzia miaka 11-15 Mambo mbalimbali yanayohusu sala na dua zake.
MAOMBI YA MTUME MUHAMMAD (S.A.W) Kutaja maombi 45 ya Mtume Muhammad (s.a.w) kwa dakika tatu.	**MAOMBI YA MTUME MUHAMMAD (S.A.W)** Atfal waliohifadhi maombi ya Mtume Muhammad (s.a.w) kuanzia namba 20-30.
HADITH NA TAFSIRI Kitabu cha **Kiunga cha watu wema** hadithi namba 98, 99 na 100.	**HADITH** 1. Kutamka hadithi 40 2. Kwa Atfal waliowahi kushiriki hadithi 40, wataulizwa namba wataje hadithi kwa matini.
HOTUBA Mada ya hotuba ni "**Mapenzi ya Masihi Aliyeahidiwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w)"**	**SHAIRI** Watapewa shairi lenye beti tano na Kughani shairi hilo. " **kiukeni kuta hizi mwingie mwangu nyumbani**" toka kitabu cha Safina ya Nuhu.
SALA YA KIISLAM Maswali ya Falsafa na Mantiki mbalimbali za vitendo vya sala. *Hekima ya sala ya Kiislamu.*	
SHAIRI KWA KHUDDAM Kutunga pamoja na Kughani shairi, Kibwagizo cha shairi kiwe ni: " ***Yarabbi swalialaa' nabiika daiman, Fihadhihidunia wabaathi Thanni"***	

Tangazo hili linaendelea uk. 9

Ulinzi wa Mwenyezi Mungu kwa Dini ya Islam

Mfasiri: Ayoub Mtekateka
Dar es Salaam

Mtukufu mtume Muhammad S.A.W alitumwa na Mwenyezi Mungu kufundisha Dini ya Islam kwa ulimwengu mzima chini ya sheria (Qurani) yenye muongozo ambayo ilikuja kuzitengua sheria zilizoletwa na Mwenyezi Mungu kupitia manabii wake waliotumwa kwa makabila na mataifa fulani maalum kulingana na mahitaji ya wakati huo. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Quran tukufu kuwa :

"Leo nimewakamilishieni (5:4) Ni dhahiri kwamba, kadri muda unavyokwenda watu nao huacha mafundisho halisi ya Dini zao. Wakati mwngine pia hata maandiko yao hupotoshwa. Ili kuulinda uislam katika maandiko na mafundisho yake kiroho, Mtume Mtukufu Muhammad S.A.W alitoa bishara kwa misingi ya funuo iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu kuilinda dini ya Islam kama inavyoripotiwa katika hadithi ifuatayo:-

"Hakika Mwenyezi Mungu atainua katika ummati huu mwanzoni mwa kila karne mtu atakaye kuja kuijadidisha dini yenu" (Abu Dawood, Kitabul Fitan)

Mbali na Wajadidi hao, Mtume Muhammad S.A.W pia alitoa bishara ya ujaji wa Mujadidi maalum ambaye pia ndiye Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa ambaye angedhihiri katika zama ambazo kutakuwa na giza la kiroho na kuenea kwa maovu. Juu ya bishara hiyo ya ufikaji wa kiongozi huyo maalum Mtume S.A.W alisema:

"Ninaapa kwa yule mungu ambaye uhai wangu upo mikononi mwake ya kwamba,masihi mwana wa mariam atadhihili kati yenu(waislam)kama hakimu muadilifu ...." (Bukhali). Pia,kudhihiri kwa Masihi huyo kulitabiriwa na Yesu kwa namna ya ufikaji wake kwa mara ya pili.

Ndani ya Qurani Tukufu,Mwenyezi Mungu ametoa ahadi ya kukilinda kitabu hicho kitukufu . Ndio kusema ya kwamba , atalilinda neno lake kutokana na makosa na kutopotea kwa herufi wala nukta yeyote ndani ya Qurani. Pia Mwenyezi Mungu ameahidi ya kwamba dini ya Islam itazishinda dini nyingine zote kwa ukweli na ubora wa mafundisho yake kama anavyosema:

"Hakika dini ya kweli mbele ya Mwenyezi Mungu ni Islam"(3:10). Na pahala pengine anasema"Hakika sisi tumeteremsha mauidha na hakika sisi ndio tuyalindao"(15:10)

Ili kuilinda Dini ya Islam, Mwenyezi mungu aliahidi kuanzisha taasisi ya ukhalifa kama ananyosema:

"Mwenyezi Mungu ameahidi wale wanye kufanya mema miongoni mwenu, Hakika atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yenu "(24:56)

Ahadi ya Mwenyezi Mungu kuilinda na kuihifadhi Qurani Tukufu imetimia kwa kiasi ambacho ndani yake zipo ishara tukufu zilizo asili ya kitabu chenyewe.ahadi hiyo ilitolewa katika mji wa makka siku za mwanzo za dini ya islam wakati mtume mtukufu Muhammad SAW na wafuasi wake wachache wako katika hatari na husuda ya maadui wa islam wakati huo.

Katika siku hizo za hatari ndipo ilipotangazwa na mwenyezi mungu kuwa makafiri hawato iangamiza quran wala hawatoweza kubadili chochote ndani yake. Mwenyezi Mungu angeiharibu mipango yao yote endapo wangetaka kufanya hivyo.

Ulinzi wa Mwenyezi Mungu juu ya Qurani Tukufu unathibitishwa hata na wakosoaji wa Islam akiwamo Mchungaji na Mwanazuoni maarufu wa Kikristo Sir William muir ambaye ameandika katika utangulizi wa kitabu chake cha '***LIFE OF MUHAMMAD***' **(MAISHA YA MUHAMMAD)** Kuwa :

"Tunaweza kuthibitisha pasipo ufedhuri kuwa kila herufi iliyopo ndani ya Qurani ni ya kipekee na si uwezo/utashi wa Muhammad mwenyewe. Kuna ulinzi wa hali ya juu ndani na nje yake,kwamba tunacho ambacho Muhammad wenyewe alikitanguliza na kukitumia. Kulinganisha maandiko yake ya asili na maandiko yetu, ni sawa na kulinganisha vitu visivyo na uhusiano "

Mwanateolojia wa kijerumani,Prof.Noldeke ameandika:

"Jitihada za wasomi wa Kimagharibi kuthibitisha uwepo wa makosa ndani ya Qurani Tukufu zimeshindikana" (Enc. Brit)

Majina ya Wajadidi ambao wamedhihiri mwanzoni mwa kila karne sawa na Aalenda ya Kiislam yameorodheshwa katika kitabu mashuhuri kiitwacho Hijajul Kiramah kilichoandikwa na Mwanazuoni Nawab Siddiq Hassan Khan aliyekuwa akiishi katika mji wa Bhopal, India. Orodha ya Wajadidi hao waliodhihiri tangu mwanzoni mwa karne ya kwanza ya kumi na tatu ni hii ifuatayo:

Karne ya kwanza – Hadhrat Omar Bin ABdulaziz wa Baghad, Iraq.

Karne ya Pili – Hadhrat Imam Mohammed Bin Idris Shaffi na Hadhrat Imam Ahmad Bin Hambal

Karne ya Tatu – Hadhrat Abu Hassan Sharh na Hadhrat Abu



Ayoub Mtekateka

Ashaie

Karne ya Nne – Hadhrat Abu Obedilla Neshapuri na Qazi Abu Bakri Baklani

Karne ya Tano – Hadhrat Imamu Ghazali

Karne ya Sita – Hadhrat Sayyid Abdulqadir Jailani

Karne ya Saba – Hadhrat Imamu Ibne Taimiyya na Hadhrat Khwaja Muinuddin Chishti

Karne ya Nane – Hadhrat Hafiz Ibne Hajal AsqalaniH na hadhrat Salleh Bin Omar

Karne ya Tisa – Hadhrat Imamu Suyuti

Karne ya Kumi – Hadhrat Muhammad Hahir Gujrat

Karne ya Kumi na Moja – Hadhrat Mujadid Alf Sani na Hadhrat Al-Sheikh Ahmad wa Sirhindi,India

Karne ya Kumi na Mbili – Hadhrat Shah Waliullah Mohaddith Dehlvi

Karne ya Kumi na Tatu – Hadhrat Ahmad Barelvi

Je, nani alikuwa mujadidi aliyedhihiri karne ya kumi na nne ambayo imekwisha mnamo tarehe 18 Novemba 1989? Kwa mujibu wa wanazuoni wa kiislamu mujadidi huyo bado hajadhihiri hilo sio jawabu. Ujaji wake umedhihiri katika dhati ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, India , ambaye si tu alidai kuwa yeye ni mujadidi Yule aliyetabiriwa na Mtume SAW, bali ndiye yule Imamu Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa. Kuhusu madai yake hayo, Hadhrat Ahmad AS anasema:

" Wakati karne ya kumi na tatu inakwisha kuashiria karne ya kumi na nne, niliambiwa na Mwenyezi Mungu kupitia ufunuo kwamba, nilikuwa Mujadidi wa karne ya 14" (Kitabul Bariya)

" Miaka michache baadaye, nilifahamishwa na Mwenyezi Mungu Kupitia ufunuo mtukufu kuwa Masihi, ambaye ujaji wake kati ya waislam ulibashiriwa mapema, na Mahdi ambaye ilikuwa adhihiri zama ambazo Uislam utakuwa katika giza la kiroho na kukithiri kwa maovu Duniani na ambaye msaada wa Mungu utakuwa pamoja naye na ambaye ilikuwa awaite watu katika dhifa za kimbingu na pia ujaji wake ulibashiriwa na Mtume SAW miaka mia tatu iliyopita ndiye mimi" (Tazkratush-Shahadatain)

"Kupitia ufunuo , Mwenyezi Mungu aeniambia ya kwamba ,nimetumwa na Mungu kama Masihi aliyeahidiwa na Mahdi na pia ni suluhishi wa tofauti za kiroho na kimaadili". (Arba'een)

Mtu fulani alimpa karatasi masihi Aliyeahidiwa AS akimtaka Masihi athibitishe kwa kiapo kuwa yeye ndiye yule Masihi Aliyeahidiwa. Alipokea karatasi lile kasha akaandika:

"Nimelisema jambo hili hapo hapo kabla katika vitabu vyangu kwa kiapo, na nina sema tena kwamba, ninaapa kwa yule Mungu ambaye uhai wangu upo mikononi mwake kwamba , mimi ndiye Masihi Aliyeahidiwa na ambaye alibashiriwa na Mtume Muhammad S.A.W katika hadithi zilizomo katika vitabu vya Sahihi Bukhari na Muslim na katika vitabu vingine vya hadithi. Allah anatosha kuwa shahidi "

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (AS) amedai bayana kwa misingi ya funuo tukufu ya kwamba yeye ndiye Mujadidi na Masihi wa karne ya 14. Amedai hivyo kwa kiapo mbele ya Mwenyezi Mungu. lazima ifahamike kuwa Qurani Tukufu na Biblia vinathibitisha kwamba wale wanaoleta madai ya uongo kuwa ni manabii wa Mungu basi Allah atawashika na kuwaadhibu . Kinyume chake ni kwamba Allah aliteremsha baraka zisizohesabika kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmadi (AS), Masihi Aliyeahidiwa wakati wa uhai wake na wakati huu ambapo jumuiya yake tukufu inaendelea kukua na kusambaa katika kila kona ya dunia huku Qurani Tukufu ikitafsiriwa zaidi ya lugha 180.Pia, Masihi Aliyeahidiwa A.S alibashiri kusambaa na kukubalika na Mataifa yote yaliyo katika kila pembe ya Dunia.

Hebu tutafakari umuhimu wa maneno haya ya mtume Muhammad S.A.W aliyopata kuyatamka karne 15 zilizopita:

"Mtakapo sikia ujaji wa mahdi ni wajibu wenu kuungana nae na hata ikibidi mtambae katika theruji kumfikia"(Kanzul Ummal)

"Yule ambaye atakufa pasipo kumtambua imamu wa zama anakufa kifo cha kijinga"(Musnad Ahmad. Vol.4)

Mwenyezi Mungu atuongoze. Amin.

Imefasiriwa kutoka Review of Religion 1990 .

MICHEZO:

Khuddam

1. **Kuvuta kamba**
2. **Mpira wa miguu**
3. **Riadha**
4. **Mieleka ya mezani kwa mikono.**

Atfal

1. **Kuvuta kamba**
2. **Kukimbia kwa magunia**
3. **Mpira wa miguu**
4. **Riadha.**

Majlis Khuddamul Ahmadiyya inawatakia maandalizi mema kwa kumtaka kila Khuddamul Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya Tanzania ajipange kuhudhuria na kushiriki kwenye Ijtmaa hiyo.

Imetolewa na:

Ofisi ya
Sadr Khuddamul Ahmadiyya Tanzania
tzkhuddam@yahoo.com

Kutoka madrasa hadi Udaktari

Kutoka uk. 11

tano katika maandalizi ya ziara ya Khalifa Mtukufu wa IV Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Waseem Ahmad Cheema alinipatia nguo nzuri akaniambia hizi utazivaa atakapokuja Khalifa kwani atakupa mkono jitahidi usikose kumpa mkono Khalifa wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ilitimia na nilifanikiwa kumpa mkono mara nyingi katika maeneo tofauti. Nakumbuka wakati wa ziara ya Khalifa Mtukufu IV hapa Masjid Salaam Dr. Iddi Mwanga ambaye alikuwa anatafsiri maelezo ya Huzur kwa Kiswahili, aliwahi kutushika mabegani mimi na Jamil Mwanga na kututambulisha kwa Huzur kuwa sisi ni watoto wake, Huzur alishika mashavu yetu kwa bashasha. Niliwahi kufika Morogoro wakati wa ziara hiyo na kushuhudia kuwekwa kwa jiwe la msingi la hospitali ya Kihonda kwa msaada mkubwa wa mzee Seleman ambaye alikuwa dereva katika msafara wa Huzur. Sikuwahi kufika Dodoma lakini nilirudi Dar es Salaam kwa gari ya marehemu Mzee Matola Nahadula aina ya 109 hadi Masjid Salaam. Katika maisha yangu ya kwenda msikitini ilifika mahala ikawa nikikosa msikitini basi ni mgonjwa au nipo shuleni. Kwani nilikuwa nafundishwa masomo mbalimbali. Nakumbuka msaada mkubwa wa kimalezi na ulinzi niliopata toka kwa Mwalimu Omari Mnungu na Mwalimu Yusuf Mbawala ambao walikuwa wanaishi pale masjid salaam. Kwa kuwa Masjid Salaam palikuwa na miti mingi ya matunda kama muembe sindano, mipera, mitini n.k, ikitokezea hakuna cha kuliwa kwa mchana hakuna udhuru wa kwenda nyumbani tunakula matunda. katika fadhila nilizopata ni kujua mti wa mtini ambao ulikuwa msikitini tu na sikuwahi kuuona mahali pengine tangu ulipotoweka pale katika sehemu nyingine hadi leo.

Sikubahatika kupata nafasi ya kuchaguliwa darasa la saba na kumpa baba yangu wakati mgumu afanye nini juu yangu kwani uwezo wangu wa kimasomo aliutambua. Wakati yeye anafikiria hivyo Mzee Mahamudi Hamsini Mubiru alishaanza kuchukua hatua za makusudi na kunitaarifu kuwa niende kwenye usahili pale Al haramain Islamic Sekondari. Katika shule hiyo pia alikuwepo ndugu mwingine wa damu ambaye alikuwa anafundisha lakini sikua namjua vizuri kabla, kwa hiyo tegemeo langu lilikuwa ni Mzee Mubiru na nikachaguliwa kupata nafasi wakati huo ilikuwa ni miongoni mwa shule bora kwa hapa Dar es Salaam kama si Tanzania nzima. Hapo nikaanza maisha mapya ya kusoma Sekondari na na juhudi yangu ilibidi niiongeze ili kuwapa imani wanaonisaidia kwenye suala la ada kwani kwa wakati huo ilikuwa kwa mwaka wa kwanza ni elfu ishirini ambayo ni nyingi mno! Baba alijitahidi mno kuhakikisha nakwenda shule na kuhudhuria masomo ya dini msikitini na alisisitiza nisikose msikitini hata iweje. Hiyo ni kweli na ndugu zangu wa kiroho walifanya kazi ya ziada kunifundisha japokuwa baadaye nilichaguliwa awamu ya pili kwenda kibasila sekondari ambako sikuweza kuhudhuria huko, naomba niwataje walimu hawa na masomo yao ambayo walinifundisha Masjid Salaam, Kiingereza ni Mahmood Hamsini Mubiru, Hisabati ni Ramzan Fazal Madhan, Physics ni Marehemu Adili Damani, Biology ni Mussa Awadh Mpinga, Commerce na Book-keeping ni Abubakari Mkoggas wale ambao sijawataja waniwe radhi si makusudi yangu.

Wakati najiandaa kwa mitihani ya kidato cha nne Hafidhu Ally Mgagi(Ndendekile) yeye alihamisha kambi toka nyumbani kwake keko na kuwa anakuja nyumbani kila siku za Jumamosi na Jumapili kuhakikisha kuwa nakuwa vizuri katika masomo yote. Wako walimu wa dini Mwl. Mbanga, Mwl. Mnungu, Mwl. Yusuf Mbawala, Mwl Mwinyimvua Ussi bila ya kumsahau Mwl. Iddi Bukhari ambaye ni Mkongo hawatasahulika kwenye kichwa changu kwa michango yao ya elimu waliyonipa iliyojaa mapenzi. Wakati wa Sheikh Naseem Ahmad Bajwa akiwa Amir Jamaat ilinilipia elfu ishirini na nne kwa ajili ya ada ya masomo yangu, fedha ilifanya kazi nzuri katika hatua za kutimiza wajibu wangu wa kimasomo. Nakumbuka maneno ya Mwalimu wangu Hamsini Mubiru aliwahi kuniambia, unaweza kuisadia Jamaat bila ya kusoma ila utakuwa unafanya kosa kubwa kama fursa ya kusoma unayo halafu unashindwa kusoma na kuisadia Jamaat vizuri zaidi, kwa kweli ni hasara kubwa. Maneno haya yalikuwa ni hamasa kubwa kwangu.

Nakumbuka nilipokuwa kidato cha nne darasa langu lilipatikana na hatia ya kinidhamu na kuamuliwa wanafunzi wote tujitetee na kuwaleta wazazi ili pia tuadhibiwe la sivyo kusimamishwa masomo kwa miezi miwili. Kwa kuwa mimi sikufanya kosa lolote na mwalimu wangu alijua fika sikuhusika akaniambia kwa kuwa ni suala la wote unabidi ufanye kama inavyotakiwa. Sikuwa na shida ya wazazi nikaenda msikitini nikamueleza Mwl. Omari naye akaandika barua nzuri na akanipeleka shuleni na Mwalimu wa nidhamu hakunipa adhabu yeyote nikarudi darasani na kuwa mwanafunzi pekee ambaye sikupata adhabu wala msukosuko wowote.

Baada ya kufanya mtihani wa kidato cha nne ukaanza mtihani mwingine wa kutafuta shule ya kidato cha tano, alikuwa tena Mwl. Mahmud Hamsini Mubiru aliyenipa ujumbe uliokwenda kwa Marehemu Mzee Burhani Mtengwa wakati huo akiwa ni mkurugenzi wa Shirika la Munadhamat Da'awa Al Islamia ambayo inamiliki Ununio High School. Hii ni katika shule bora za wakati huo katika mchepuo wa PCB na kwa kweli kwa ujumbe ule sikuwahi kuulizwa ada hata siku moja na nikasoma hadi kidato cha sita na kumaliza masomo. Katika kipindi hiki nawakumbuka sana ndugu zangu akina Mussa Mpinga na wengine ambao walihakikisha maisha yangu ya shuleni yanaenda sawa kwa kunipatia fedha muhimu kwa maisha ya shule, Bwana Hafidhu Mgagi aliendelea kuwa mwalimu wangu wa uhakika katika masomo hayo na elimu yangu ya juu ya sekondari vizuri.

Matokeo yangu ya kidato cha sita yaliniwezesha kupata nafasi ya Wizara ya Afya katika Chuo cha Maafisa Tabibu Kibaha na hapa ni kazi nzuri sana iliyofanywa na ndugu mbalimbali katika Jumuiya hii. Ndugu hawa wakiongozwa na Marehemu Ramadhani Marunda ambaye alilipa ada yote ya kozi yangu hiyo na hivyo kuwa sehemu muhimu sana ya mafanikio hayo ya kielimu kwa wakati ule. Kaka Mussa Mpinga wakati naenda Kibaha alinielekeza kwa ndugu wa Kibaha ambako pia nilipata ulinzi, mapenzi ya kindugu na hata kutembelewa chuoni na Bwana Abdulrahmani Malinda ambaye alikuwa hakosi zawadi akija kuniona.

Nilimaliza masomo vizuri na baada ya muda wa mwaka mmoja wa kufanya kazi zahanati binafsi Mlandizi nikapata ajira ya Serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na kupangiwa kituo cha Afya Ikwiriri nikiwa Afisa Tabibu Daraja la II. Huko nilikutana na ndugu zangu wengi ambao waliimarisha imani yangu. Nilimkuta Mzee Matimbwa Ngobo akiwa peke yake na Jamhuri Kahewanga wakipambana na masuni katika hali ya ajabu, kikosi kiliongezeka tulichofanya Mwenyezi Mungu anajua zaidi. Baada ya miaka miwili, Nikapata uhamisho wa kuhamia Kituo cha Afya Kibiti uhamisho ambao ndugu zangu wa kibiti walikuwa wanaungoja kwa hamu. Bwana Yusuf Shaabani Malinda Rais wa Jamaat Kibiti alituma gari yake kunihamisha na kunipa nyumba yake mpya nifanye makazi jambo ambalo wafanyakazi wengi wa serikali ni nadra kupata hayo. Uhamisho huo ambao watu wanasema haijawahi kutokea kwa daktari kutoka Ikwiriri kuhamishiwa kibiti katika historia ya Halmashauri hiyo sababu zake bado anazijua Mwenyezi Mungu vizuri zaidi. Maisha ya Kibiti kwa upande wa Jamaat yalikuwa mazuri chini ya malezi ya Sheikh Kambaulaya ambaye ni baba yangu mwingine wa kiroho na mwenye mapenzi makubwa nami.

Baada ya miaka miwili ya kuishi Kibiti nikapata nafasi ya kwenda kusoma zaidi, jambo ambalo Marehemu Mzee Kitabu Pazi lilikuwa ndiyo ndoto zake kwani nakumbuka aliwahi kuniambia " jitahidi upate degree ya udaktari ili uisaidie vizuri Jumuiya na familia" na aliwahi kuniambia "nakuona mwanangu una mzigo mkubwa wa Jamaat na familia uko mbele yako hivyo soma sana baba". Masomo yalikuwa ni miaka mitano ambayo ada yake pia ilikuwa nyingi kwangu. Hapa pia Mwl. Mahamudi Hamsini Mubiru alifanya kila jitihada ili nisishindwe kusoma, akiwemo Mzee Alli Said Mosse, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaundry na ndugu wengine wengi na hatimaye nikapata msaada wa kulipiwa sehemu ya ada dola elfu tisa kutoka kwa baba wa kiroho, Hadhrat Khalifatul Masih V, Mirza Masroor Ahmad (Mwenyezi Mungu aampe nguvu na umri mrefu). Namshukuru Kiongozi huyu wa kiroho kwa haya yote kupitia Ukhalifa wetu huu na kwa sasa nafanya kazi Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Sina fadhila ya kulipa kwa wanajumuiya na Jumuiya kwa yote ambayo nimefanyiwa katika malezi mbalimbali na hatua za kielimu nilizopitia. Namuomba Mwenyezi Mungu alinde imani yangu ili na mimi niwe sehemu ya watu watakaotajwa katika maendeleo ya ndugu wengine katika Jumuiya yetu hii, kubwa zaidi naomba kwa Mwenyezi Mungu nipate mwisho mwema.

Amin.

SHURA YA KITAIFA 2013

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2012/13 Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 27 - 28 April 2013.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 26 April 2013.

Ni muhimu kila tawi la Jumuiya lisipoteze nafasi yake ya kuleta mjumbe kwani wakati wa Shura hiyo pia kutakuwa na uchaguzi wa Majlis Amila ya Taifa.

Sakata la Kuchinja wanyama

Kutoka uk. 12

wasome maneno matakatifu ya Biblia katika kitabu cha Yoshua Bin Sita yanayosema kwamba; "Alaaniwe mtu mchongezi na mdanganyifu, maana amewaangamiza wengi wanaoishi kwa amani, uchongezi umevunja amani ya wengi na kuwatawanya kutoka taifa hata taifa lingine, uchongezi umeangamiza miji yenye nguvu, na kuangusha nyumba za wakuu. Uchongezi umewafanya wake za waaminifu wawakimbie waume zao, na kuwanyang'anya matunda ya jasholao,yeyoteanayemsikiliza mchongezi hatatulia moyoni, wala hataishi kwa amani. Pigo la mjeledi hubakiza kovu, lakini pigo la ulimi huvunja vunja mifupa, watu wengi wameuawa kwa upanga, lakini wengi zaidi wameuawa kwa ulimi, heri mtu ambaye amekingwa mbali na ulimi". (Kwa maelezo zaidi soma kitabu cha Yoshua Mwana wa Sita 28:13 - 19).

Maneno hayo ya hapo juu kutoka kwa Yoshua Mwana wa Sita yanaeleza kwa uwazi kabisa nasaha kwa Maaskofu kwamba wawe waangalifu katika kutoa kauli na matamshi yao mbele ya Waumini wao, watowe kauli na maneno yenye kuleta amani na maelewano kwenye jamii sio kauli mbaya zitakazohamasisha kuleta fujo, vurugu na kutoelewana. Kwa sababu Waumini wao Wakristo walihamasika wakaanza kuchinja nyama mara tu baada ya kusikia tamko la Baraza la Maaskofu linalowataka waumini hao Wakristo kwamba wasusie kununua nyama na Waislam, hapo ndipo vurugu zilipoanza kutokea baina ya Waislam na Wakristo.

Pia Mtakatifu Paulo anawaambia Maaskofu kwamba, "Msemo huu ni wa kweli; Mtu anayetaka kuwa Askofu, huyo anatamani kazi nzuri. Basi, Askofu anapaswa kuwa mtu asiye na lawama, anapaswa kuwa na mke mmoja tu, awe mwenye kiasi, nidhamu na utaratibu, ni lazima awe mkarimu na anayeweza kufundisha, asiwe mlevi au mtu wa matata, bali awe mpole apendaye AMANI. (1 Timotheo 3:1-3).

Pia maneno hayo ya hapo juu ya Mtakatifu Paulo anawausia na kuwataka viongozi hasa wa Kikristo wakiwemo na Maaskofu kwamba wawe watu wa amani, nidhamu, wapole, wasiwe wachonganishi katika jamii. Hivyo basi haikupendeza kuona waheshimiwa Maaskofu hasa wa Mwanza, badala



Mwl. Kais Ally

ya kuhimiza amani, wao wanachochea Waumini wao Wakristo wasusue kununua nyama zilizochinjwa na Waislamu na kuwachochea waumini wao kufanya fujo.

Madai yao kusema kuwa wanasusia nyama zilizochinjwa na Waislam kwa kuwa zimechinjwa kinyume na misingi ya imani yao hayaonekani kuwa na mashiko, kwani hakuna sheria yoyote wala muongozo wowote kwa mujibu wa kitabu Kitakatifu cha Biblia kuhusiana na suala la kuchinja. Aidha kimsingi tamko la Serikali lililofafanuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu linamaanisha hivyo kuwa Wakristo hawana sheria yoyote inayowaongoza kuhusiana na uchinjaji.

Hivyo tunawasihi sana Maaskofu hususan wa kule Mwanza kushikamana na mafundisho ya Mtakatifu Paulo yaliyoelezwa hapo juu. Ni vyema wasimamishe amani na kuhimiza amani kuliko kuchochea vurugu ambazo hazina manufaa yoyote kwa wao wenyewe wala kwa Waumini wao bali ni hasara kwa Taifa letu lililojulikana kwa miaka mingi kuwa ni kisiwa cha amani.

Aidha kwa upande mwingine tunavilaani vitendo vilivyofanywa na Waislam wa kijiji cha Buselesele cha kwenda kuvamia Bucha ya Mkristo na kuanza kuleta fujo na vurugu zilizosababisha kuvunjika kwa amani. Matendo ya namna hiyo hayakubaliki na mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam. Mwenyezi Mungu Anasema katika Qur'an Tukufu kwamba "Wala Msifanye uharibifu (fujo) katika nchi ikiishatulia, na Mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumaini. Bila shaka Rehema za Mwenyezi Mungu zi karibu na wafanyao hisani. (Qur'an sura ya 7:57).

Tena Mwenyezi Mungu Anasema kwamba; "Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, na hisani na kuwapa watu kama uwapavyo ndugu, na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu". (Qur'an Sura 16:91).

Tena Mwenyezi Mungu Anasema; "Na Mwenyezi Mungu Hapendi uharibifu" (Qur'an 2:206). Ndugu wasomaji wapendwa aya hizo hapo juu zinawakataza Waislamu na wanadamu kwa jumla kufanya fujo na vurugu. Kwa mantiki hiyo Waislamu kwa vyovyote wamekatazwa kufanya fujo na vurugu za aina yeyote ile, Waislam wanatakiwa wafahamu kuwa Islamu sio dini ya vurugu na fujo bali ni dini ya amani, subira na maelewano, hivyo basi ni vizuri Waislam wote duniani wakaishi na ndugu zao wasiokuwa Waislamu kwa wema, amani, huruma na maelewano kwani ndivyo mafundisho ya dini tukufu ya Islamu yanavyowataka Waislam wawe watu wa amani na ndivyo alivyofundisha Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na neno Islam maana yake ni amani, utii na unyenyekevu.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Kutoka Chekechea hadi Udaktari

Kutoka uk. 12

alinikabidhi kwa wazee wangu wawili ambao walikuwa wananifundisha Yasarnal Qur'aan, kwa kuwa ni siku nyingi huenda wenyewe wamesahau nao ni Mzee Shaabani Zonga na Mzee Athumani Mgalu kwa bahati hawa pia ni wazee waliokuwa karibu sana na Mzee kwa hiyo nikawa nimefika. Wazee wangu walinipenda sana na kuthibitisha hilo wazee hawa kwa nyakati tofauti baada ya kuona nimemaliza masomo walinifuata ili nioe mabinti zao, ni kwa ajili ya mapenzi waliyonayo kwangu. Kwa kuwa idadi ya mabinti ni kubwa haikuwa rahisi kuoa wote hivyo nikaanza na mmoja. Wakati wa utoto wangu Ilikuwa kila siku ni lazima nifike msikitini kwanza na ndiyo naenda nyumbani kwani nina uhakika wa kusoma Yasrnal, kuonana na watu niliowazoea na sitokaa na njaa. Baadhi ya siku nikirudi nyumbani baada ya sala ya alasiri chakula cha wote kinakuwa bado wakati tayari mimi nimeshiba. Hii ikaniongezea jazba kuwa ukienda msikitini kuna faida nyingi sana ikiwemo kutoshinda na njaa. Kutokana na umri wangu kuwa mdogo nilikuwa nikipata ulinzi wa hali ya juu kwa usalama wangu, japokuwa kuwa miaka ile magari hayakuwa mengi hapa Dar es Salaam, lakini kwa umri wangu na Mapenzi ya ndugu zangu walihakikisha wananifikisha nyumbani na wao waendelee na safari zao. Namkumbuka kaka yangu Marehemu Jafari Maliki Mahamba (Mtoboa siri) alikuwa akifanya kazi hii mara nyingi sana na siku asiponiona msikitini anafunga safari kuniulizia kwa mama Kariakoo na kunisubiri hadi anione hata kama nilichelewa kutoka shuleni. Kaka wengine waliofanya kazi hii ni Marehemu Adili Damani akiwa anasoma Chuo cha Ardhi, alikuwepo Mussa Awadhi Mpinga wakati huo akiwa anasoma Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili, Ramzan Fazal Madhan akiwa anasoma chuo cha Ardhi, nimewataja wachache kwani orodha ni ndefu na nachelea nafasi haitoshi. Wapo wazee wangu waliofanya kazi hii ya kuhakikisha nafika salama nyumbani, naikumbuka baiskeli iliyoandikwa Mke si mali fanya kazi inayomilikiwa na Mzee Ramadhan Athumani Shamte (Akili si mali) imenipeleka mara nyingi nyumbani na kunikabidhi kwa mama ndiyo anaanza safari ya kwenda nyumbani kwake Kinondoni. Mzee wangu Marehemu Mohamedi Saidi wa Kivukoni (Mwenyezi Mungu amlaze pema) amefanya shughuli hii sana. Wapo babu zangu ambao hawakuwa nyuma kwani Marehemu Mzee Rashid Msabaha na Mzee Idd Ramadhan walikuwa wakinipeleka nyumbani kwa mwendo wao wa taratibu, mwendo ambao mimi nilikuwa naona wananichelewesha kwani nataka kukimbia lakini nakumbuka siku moja Mzee Rashidi Msabaha nilimpita kwa hatua kadhaa akaniita Ya Swaleh! "Waongozanapo wawili si vyema ukamwachia mwenzio polepole ndiyo mwendo."nakumbuka kauli hii ya Mzee huyu aliyekuwa na sifa nyingi za utawa. Aidha nakumbuka siku moja nilikuwa naongoza na Mzee Rashid Msabaha tukafika makutano ya Mtaa wa Kongo na Tandamti nikaanza kupiga mruzi katika ile michezo ya kitoto, Mzee Msabaha alisimama kunisikiliza kwanza nilipomaliza akaniambia nataka ukariri sasa hivi aya hii *"wamakana salat him I'ddal bayti ila muka'a wataswidyattan fadhuukul adhaba bimakuntum takfruun."* Tafsiri ni " haikuwa sala kwao kwenye nyumba ila miruzi na makofi basi onjeni adhabu kwa yale mliyokufuru". Nikawa nasoma huku tunatembea huku ananikariri sha pamoja na tafsiri alifanya hivyo mara tatu mpaka tunafika kona ya mtaa wa Tandamti na Msimbazi hiyo kazi ikawa imekwisha na nikawa nasoma mwenyewe hadi nyumbani aliponiacha. Siku hiyo ndiyo ulikuwa msemo wangu kwani hiyo tabia ilikuwa sana miongoni mwa watoto wengi pale mtaani kwa hili nilisaidia sana kupunguza miruzi pale maeneo ya nyumbani. Kesho tulipoonana aliniuliza "je umeelewa maana ya aya ile" nikamwambia kupiga miruzi ni vibaya kwani watu wanafanyia ibada na hiyo ni kufuru kubwa, akajibu barabara mjukuu wangu. Huyo ndiye Rashidi Msabaha ambaye pia nitamkumbuka kwa tabia yake ya kusali sala dhuha mara aingiapo msikiti asubuhi, alijaa upole, unyenyekevu na adabu kwa watu ambaye pia ni Mtanzania pekee ambaye si mbashiri aliyewahi kumuona Khalifa wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa alipokwenda Qadian. Kwa kweli wapo wazee wangu wengi waliofanya kazi hii ya malezi kwangu na sirahisi kuwataja wote hapa, ila kwa uchache ni Marehemu Ally Salum Ndendekile, Mzee Sultani Ungando, Marehemu Mohamed Ussi, Marehemu Al Haji Kungulilo, marehemu Mohamed Kagoi, Marehemu Mustafa Kapulilo, Mzee Othumani Ungele, Mzee Mohamed Said Kibindu, Mzee Khamis Sultan Wamwera, Marehemu Iddi Ramadhani n.k.

Mzee Iddi Ramadhan alikuwa akinipeleka nyumbani lakini kwanza tupite kwa Sheikh Nurdin Hussein Shadhiry tukamhubiri. Ilikuwa ni kawaida yake kutembea na vitabu mbalimbali na kwa kweli nyumbani kwake pale Mtaa wa Swahili palikuwa hakuna mahala pa kukaa kwani kote kumejaa vitabu. Vitabu vilikuwa kwenye viti hadi mchagoni. Huyu ni Mzee aliyenifundisha kuthamini vitabu vya Jumuiya. Aliwahi kunipatia baadhi ya vitabu vyake zawadi. Alikuwa ananipenda sana na nakumbuka siku moja alinipeleka nyumbani na wakati anaondoka nikaanza kumsindikiza hadi kwake mtaa wa Swahili halafu akanirudisha tena nyumbani. Hawa ndiyo baba na babu alioniambia Marehemu Mzee Kitabu Pazi. Nakumbuka wakati nasoma darasa la

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jumadul awwal 1434 AH | Machi 2013 | Amman 1392 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Kuna maombi ya aina tatu ambayo hupokelewa bila wasiwasi. Ombi la aliyedhulumiwa, ombi la msafiri na ombi la baba kumwombea mwanawe. (*Tirmidhi*)

Sakata la Kuchinja wanyama

- ***Nani mwenye uhalali wa kuchinja; Mwislamu au Mkristo?***
- ***Viongozi wa dini acheni kuwapotosha watu.***
- ***Serikali iwe macho na viongozi wa dini wanaotaka kuchochea chuki na vurugu***

Na Mwalimu Kais Ali, Mkongotema Jamaat Madaba Songea.

Hivi karibuni sawa na taarifa kutoka kwenye vyomba vya habari tarehe 12/02/2013 katika kijiji cha Buselesele Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita kulitokea vurugu kubwa sana zilizopelekea kutoweka kwa amani kiasi ambacho kulitokea na mauaji kwa Mchungaji wa Kanisa la Pentekost Assembles of God Bw. Mathayo Kachila na watu wengine 16 walijeruhiwa na kulazwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Chato. Inasemekana hali zao zinaendelea vizuri. Mapigano hayo yalifanyika kati ya waumini wa dini ya Kikristo na Waislam.

Kwanza natoa pole kwa waathirika wa mkasa huo hasa kwa wale walioumizwa katika pande zote yaani kwa Waislam na Wakristo pia namuomba Mwenyezi Mungu Amsamehe makosa yake Mchungaji Bw. Mathayo Kachila aliyefariki kwa ajili ya vurugu hizo.

Ifahamike kwamba vurugu hizo zilianzia muda mrefu mwaka jana Mwezi disemba 2012, katika Wilaya ya Sengerema Mkoa wa Mwanza yalifanyika mabishano hayo ya uchinjaji wa nyama na kupelekea Mwenyekiti wa Ulinzi wa amani katika Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ndugu Evarist Ndikilo aliitisha mkutano katika Wilaya ya Sengerema na kutoa tamko la Serikali kwamba wenye uhalali wa kuchinja nyama kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, n.k ni Waislam tu. Pia tarehe 30/01/2013 Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni Mheshimiwa Waziri Mkuu Ndugu Peter Pinda akiwa Dodoma alikohudhuria kikao cha Bunge naye pia alitoa tamko la serekali alipozungumza na Waandishi wa habari kwamba; "Kwa Muda mrefu imezoeleka wanaochinja nyama (halali) ni Waislam, kwa sababu wao Waislam ndio wanayo sheria ya kuchinja wanyama, lakini sisi Wakristo hatuna sheria hiyo ya kuchinja".

Mara baada ya kutokea kwa vurugu hizo zilizopelekea mauaji Mheshimiwa Waziri Mkuu alilazimika kufunga safari kwenda Wilayani Chato kushughulikia mgogoro huo. Alifanikiwa kuzungumza na viongozi wa dini wa pande zote mbili yaani Waislam na Wakristo lakini inaonekana kikao hicho hakikuwa na ufanisi mzuri sana. Ndipo tarehe 16/01/2013 Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati yupo Wilayani Chato alizungumza na Waandishi wa habari na hapo pia akatoa tamko la Serikali kwamba, "Kuhusu kuchinja wanyama halali yaani kama vile ng'ombe, n.k uendelee utaratibu uleule wa zamani, yaani wachinjaji wawe ni Waislam tu, mpaka pale utakapoanzishwa utaratibu mpya".

Kinachosikitisha ni pale ambapo waheshimiwa Baraza la Maaskofu Mkoa wa Mwanza kwa makusudi waliamua kuuzima moto kwa mafuta ya petrol pale walipothubutu kutoa tamko la Baraza la Maaskofu kwamba, "Baraza la Maaskofu linatamka kwamba Wakristo wote wasiende kununua nyama zilizochinjwa kinyume cha imani yao". Kwa tamko hilo Maaskofu wanamaanisha kwamba nyama zote zinazochinjwa na Waislam wanawaambia Waumini wao Wakristo wasisiende kuzinunua popote ziuzwapo kwenya maduka ya nyama.

Tamko la Maaskofu linahuzunisha mno, kwa sababu Maaskofu walikuwa wanafahamu wazi kwamba nini kitakachofuata baada ya wao kutoa tamko lao hilo, kweli walichokitaka kikatimia. Fujo na ghasia za hali ya juu zilizotokea zilizosababisha kifo cha Mchungaji Bw. Mathayo Kachila. Pengine ni matokeo ya mbegu mbaya ya chuki iliyopandwa na Waheshimiwa Maaskofu wa Mwanza. Kwa sababu kauli ya kuwataka Waumini wao Wakristo wasusie kununua nyama zilizochinjwa na Waislam kwa madai zimechinjwa kinyume na imani yao, zimewafanya Waumini wao kudhani kwamba jambo la kuchinja ni la kawaida na hata wao Wakristo wanaweza kuchinja bila tatizo lolote lile.

Wakati Maaskofu wanafahamu kwamba Waislamu wanapochinja wanafuata amri ya Mwenyezi Mungu iliyomo ndani ya Qur'an Tukufu. Ilhali wao Wakristo hawana amri yoyote ya Biblia inayozungumzia utaratibu wa kuchinja wanyama. Habari zinaeleza kwamba chanzo cha vurugu hizo ni pale ambapo Mkristo mmoja wa Buselesele (Chato) alipoamua kuchinja nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo na akaenda kuuiuza katika bucha lake, ndipo Waislam walipomfuata kwenda kumuhoji ghafla fujo zikaanza kutokea. Ingawa haikufahamika tatizo ilikuwa nini mpaka vurugu zikazuka.

Historia ya Maaskofu katika nchi ya Rwanda sio nzuri. Inasemekana kwamba Maaskofu wa Kikristo walitoa mchango mubwa sana katika mauaji ya vita vya kimbari vilivyopiganwa kati ya makabila mawili yaliyo ndugu yaani Wahutu na Watusi. Inasemekana Maaskofu walikuwa wanatumia matamko na kauli za uchochezi kuwahamasisha watu wa kabila jingine wawauwe wenzao wa kabila jingine.

Hivyo basi ninaiomba Serikali yetu hivi sasa iwe macho na viongozi wa dini wanaotaka kutumia kauli zao na matamko ili kuchochea waumini wao ili kutaka kuchafua amani ya nchi yetu iliyodumu zaidi ya miaka hamsini na moja iliyopita. Maaskofu wanatakiwa

Endelea uk. 11

Kutoka Chekechea hadi Udaktari

Na: Pazi Kitabu Mazongera Dar es Salaam.



Dr. Pazi siku ya kuhitimu shahada ya Udaktari

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kueleza machache juu ya msaada wa kielimu nilioupata kutoka kwenye Jumuiya yangu na wanajumuiya kwa ujumla hadi hapa nilipofikia.

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuitambua Jumuiya hii hasa ukizingatia mahali nilipozaliwa pale Kariakoo. Nilipelekwa shule ya Chekechea Msimbazi Polisi. Nikisema Kariakoo wako wanaofahamu maana yake ni nini. Wako niliozaliwa na kukua nao pamoja leo wamefungwa jela kwa makosa mbalimbali, wako wanaotumia na kuathirika kwa madawa ya kulevya, wako waliochanganyikiwa akili kwa matumizi ya bangi na wako pia waliopoteza maisha kwa makosa mbalimbali, kwa sababu hizi nimefika hapa si kwa ujanja wangu bali ni kwa msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu ambao nina kila sababu ya kuushukuru. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi kwa kunijaalia wazazi (hapa ndipo nilipokwama kwani nilikumbuka mengi kwa sekunde chache na kuona sura ya marehemu baba mbele yangu ikiwa na tabasamu na kushindwa kuendelea na maelezo yangu. Nawaomba radhi wale wote niliowapatia huzuni hii na kukosa utulivu kwa tukio lile ambalo lilikuwa nje ya uwezo wangu) hususan baba ambaye ameikubali na kuielewa Jumuiya hii kwani aliwahi kuniambia kuwa mwanangu shikamana sana na Jumuiya kwani mimi ni kama nipo peke yangu ndugu zangu ni watoto wangu lakini ukiwa ndani ya Jumuiya hata kama mimi nikifa utapata baba wengi, mama wengi, shangazi wengi, wajomba wengi, kaka zako wamejaa tele na wewe hutakuwa mkiwa Abadan. Maneno haya aliniambia nikiwa na miaka saba na akayarudia siku ambayo alifariki dunia tarehe 7 Disemba 2002 katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Ni yeye aliyefanya ushawishi wa makusudi nikiwa mtoto wake ili nipende msikiti kwa kunipa kila nilichohitaji nikiwa naelekea masjid Salaam. Alihakikisha Napata chai ya hotelini na chakula cha hotelini ili nisisubiri chakula cha nyumbani kwani huenda nikachelewa msikitini. Alinijengea mapenzi ya kupenda msikiti kwa kunihimiza kusoma na kwa kuhakikisha nafanya hivyo

Endelea uk. 11